

KUPOROMOKA KWA ULIMWENGU



Asante sana, Ndugu Neville.

Habari za asubuhi, marafiki. Niliijengeuzageuza tu kitandani asubuhi ya leo kwenye wakati wa kuamka tena nitoke, basi nilikuwa kidogo nimechoka. Sikuja...kwa namna fulani nilikuja bila kutarajiwa. Ndugu Shakarian, Wafanya Biashara wa Full Gospel, rais wa shirika hili, alikuwa...Mkewe alikuwa ni mgonjwa, na kwa hiyo...naye alipelekwa hospitali.

² Na kusimama badala ya mtu kama huyo ni kibarua kikubwa, na kuuendesha mkutano jana.

³ Na Ndugu Arganbright alipitia hapo, na tukapanda juu. Na, vema, niliamka saa kumi, jana asubuhi, na tukaanza safari kwenda Cincinnati. Na tulikuwa tunasafiri siku nzima. Ndipo nikaingia, nikaingia tu. Tuliingia karibu mapambazuko, asubuhi ya leo. Na kwa hiyo ni mchovu, na nimepwelewa na sauti, lakini tupo hapa kwa neema ya Mungu.

⁴ Sijui kama Ndugu Arganbright alifaulu. Je! upo hapa, Ndugu Arganbright? Hapana shaka angali mikononi mwa Morpheus. Hamjui Morpheus alikuwa ni nani; alikuwa ni mungu wa kikafiri wa Kirumi, mungu wa usingizi.

⁵ Kwa hiyo nyote mnivumilie kidogo kwa kupwelewa kwangu na koo asubuhi ya leo, nami nitajaribu kutowashikilia kirefu mno.

⁶ Kusudi langu la kufanya ibada asubuhi ya leo lilikuwa ni kwa sababu ya...sio watu. Jumapili ijayo nilikuwa niutoe ujumbe wa—wangu wa Krismasi, lakini, kama ni—ningeutoa, basi ungewaleta watu wanaotoka nje ya mji, labda kwa namna fulani ukatize Krismasi yao, mwajua, ya kurudi. Na kwa hiyo nikawazia labda lingekuwa ni jambo jema sana kama tukikusanyika pamoja na kumwabudu Bwana asubuhi ya leo, kwa njia hii, kwa sehemu yangu ya ibada ya Krismasi. Na halafu Jumapili ijayo mngekuwa kwenye ninii yenu...Kama unaishi mbali, ungeweza kuwa kwenye kanisa lako mwenyewe popote unapotoka, ama lolote unalotaka kufanya.

⁷ Nami ninataka kumshukuru ndugu huyu kwa wimbo huo mzuri. Niliingia tu wakati ulipokuwa ukiimbwa. Huo ni mzuri sana. Na wakati wote nimemsikia mke wangu na hao wote wakijivunia uimbaji wa ndugu huyu, na nilikuwa na nafasi yangu ya kwanza kumsikia akiimba, mimi mwenyewe, nje ya maskani. Sasa, hilo si ni la ajabu? Ndugu yetu wa hapa maskanini, na ilinibidi kwenda mpaka Shreveport, Louisiana, kumsikia akiimba wimbo wake wa kwanza. Jinsi mambo yalivyo ya ajabu, sivyo?

⁸ Na halafu tuliwazia labda kwamba kufanya jambo hili, lingetupa wakati katika ninii yetu...wa—wa kukusanyika pamoja. Halafu tena barabara zilikuwa ni mbaya sana. Sijui kama Ndugu na Dada Dauch walifanikiwa kutoka Ohio. Je! walikuja? Uko wapi, Ndugu Dauch? Naam, naam. Nilikuwa nikishangaa tu. Je! mna theluji nyingi sana huko? Theluji nyingi sana. Kwa hiyo, vema, hawakuwa na yoyote Cincinnati. Hata hakuna kama ilivyo hapa. Hata hakuna theluji hata kidogo. Na mara ya kwanza niliyopata kuhubiri Cincinnati ilikuwa ni jana, na kwa hiyo tulikuwa na siku nzuri, tawi jipya ambalo halijamaliza mwaka mmoja, na ni tawi zuri sana, watu wazuri. Tulifurahia ushirika huo. Basi wao wamepiga simu sasa hivi kwamba niwepo Columbus kesho, kwa ajili ya kuwekwa wakfu kwa tawi lingine, na, ama ibada, ambayo Ndugu Shakarian alipaswa kuichukua, lakini...nami sina budi kuombea jambo hilo kwanza. Ni ninii...

⁹ Inanibidi kwenda Phoenix mara baada ya hapa, mwajua, nasi tuna...Tunaanzia huko Phoenix tarehe kumi na mbili, itakuwa ni kiamshakinywa cha wafanya biashara. Na sijui mahali unapofanyiwa. Nafikiri ni kwenye Ramada, utafanyiwa Ra—Ramada. Lile tawi la wafanya biashara lina kiamshakinywa chao cha kawaida hapo. Na halafu Jumapili nitaanza kwenye, na Jumapili, kwa karibu siku kumi na mbili kila mahali kote katika Bonde la Marikopa, Phoenix, Tucson. Nami nina dhifa Jumatatu usiku, Jumatatu inayofuata usiku, huko Tucson, dhi—dhifa pamoja na wahudumu na Wafanya Biashara wa Full Gospel huko Tucson. Na ndipo basi nirudi Phoenix, nami nafikiri ni huko Glendale na mahali mbalimbali. Na basi mkutano unaanza tarehe ishirini na...Ni nini, Ndugu Fred? Unakumbuka ninii... Ishirini na nne, ishirini na nne hadi ishirini na nane ama ishirini na tisa, kitu kama tarehe hizo. Halafu basi, Bwana akipenda, nitarudi nyumbani. Tutaona jinsi ambavyo tumeendelea hapa, tuone kuhusu ile Mihuri Saba ama ninii...tangu wakati huo na kuendelea, na tuone mahali tutakapoenda kutoka hapo.

¹⁰ Sasa, naamini mtu fulani aliniambia tulikuwa na watoto wachanga hapa asubuhi ya leo wa kuwekwa wakfu. Hiyo ni kweli? Je! yupo mama aliye na mtoto wa kuwekwa wakfu? Jambo fulani aliloniambia Dak. Vema, labda nilikosea. Loo, ndiyo. Naam. Ndiyo, bwana, hawa. Vema, ninyi dada ama ndugu mwaweza kuwaleta watoto wenu huku? Asante, dada. Nafikiri huu ni wakati mzuri sana wa kuwaleta watoto, ni Krismasi. Ndugu Neville, waweza? Sasa, wakati wapendwa hawa wanapowaleta watoto wao wadogo asubuhi ya leo, ni—ni ninii tu...

¹¹ Sasa, watu wengi, katika makanisa mengi, na—na kama yeyote wenu alikuwa mkutanoni jana, jinsi ambavyo Ndugu Brown, Mweskopolia aliyejazwa na Roho Mtakatifu, akiwaomba radhi waaminio wa Kipentekoste, juu ya kuwabatiza watoto

wachanga, kwa hiyo, kabla ya kusema yale aliyotaka kusema. Kwa hiyo Mweskopolia hubatiza, kwa kunyunyizia, wanaoita ubatizo.

Batiza, kwangu mimi, linamaanisha “kuzamisha, kuingia chini, mazishi.”

¹² Na, lakini wengi wao hufanya jambo hilo. Hilo ni ninii la kale...Huo ni mtindo ambao kweli ulitokana na kanisa Katoliki, nao ukaingizwa kwa Methodisti na Episkopolia, Lutheri na wengi wao hufanya hivyo. Wamethodisti hufanya hivyo. Huo ndio uliokuwa utengano kati ya kanisa la Nazarayo na la Methodisti, ilikuwa ni ubatizo wa watoto wachanga. Mnazarayo ni Mmethodisti kwa kila neno, ila tu kwa ubatizo wa watoto wachanga, na kwa hivyo lilijitenga kwa kusudi hilo.

¹³ Church of Christ ni Kanisa la Kikristo, kila kitu ila muziki kanisani. Na kwa hiyo, loo, masuala hayo madogomadogo ambayo wanatengana na kuvunjilia mbali udugu na kadhalika! Sisi sote ni mmoja katika Kristo Yesu, kwa...Huwezi kujiunga na kanisa. U—unajiunga na nyumba ya wanachama, bali huwezi kujiunga na kanisa, unaona, kwa kuwa huna budi kuzaliwa katika kanisa. Ni kuzaliwa kiroho. Na kwa hiyo madhehebu mbalimbali yana mawazo yao na, tunaambatana tu nao, hivyo tu.

¹⁴ Lakini kwe—kwetu sisi hapa maskanini, tunataka kukaa vile vile hasa Biblia inavyosema lifanywe. Kile tu...Wala hakuna Andiko katika Biblia la kumbatiza mtoto mchanga. Hakuna Andiko katika Biblia la kunyunyizia. Na kwa hiyo Andiko pekee lililopo katika Biblia ambapo Yesu alisema jambo hilo, Yeye alikuwa Ndiye Kielelezo chetu, na wakati walipomletea watoto Yeye aliweka mikono Yake juu yao akawabariki, na kusema, “Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwakataze, kwa kuwa walio kama hao Ufalme wa Mungu ni wao.” Sasa, hivyo ndivyo tunavyojaribu kuendelea.

¹⁵ Sasa, tunajua, wakati mimi pamoja na mchungaji tunapoweka mikono juu ya watoto hawa wachanga, mikono yetu ni kabadala duni cha Bwana wetu, kwa kuwa Yake ilikuwa ni mitakatifu. Lakini kama ingalimbidi kutafuta kote duniani asubuhi ya leo kuupata mkono mtakatifu, ungeupata wapi? Hakuna kitu kama hicho, unaona, duniani. Lakini kwa neema Yake tunamwakilisha. Na watoto hapa tutakaokuwa tukiwaweka wakfu, tutaweka mikono yetu juu yao na kuomba maombi na shukrani kwa kuwa amewaleta kwa watu hawa, na wawe maua nyumbani mwenu ya kusaidia kuwaangazia njia mnaposafiri. Naomba walelewe katika maonyo ya Mungu. Na watoto hawa wadogo na wawe sasa wafanya kazi hodari, kukiweko na kesho, katika Ufalme wa Mungu, ndiyo maombi yetu maaminifu. Vema. Bwana na abariki.

¹⁶ Hebu tuone, ninaamini tutaanzia hapa, kwa jamaa huyu mdogo, mwenye nywele nyeusi anayenikazia macho sana. Kwa namna fulani tu... Loo, jamani! Mke wangu anapaswa kuwa hapa kumshika mtoto huyu mdogo. Daima mimi nahofu nitawavunja, mnaona. Jamani, ni mtoto mzuri jinsi gani! U hali gani? Ni wakati unaofaa jinsi gani, wakati, “Katika hori, Mtoto alionekana,” wakati wa Krismasi, kwa ajili ya kuwaweka watoto wakfu kwa Mungu. Jina lake ni nani? Samuel Thomas. Sasa, hilo ni jina zuri sana.

Na tuviinamishe vichwa vyetu.

¹⁷ Baba yetu wa Mbinguni, wakati maskini mume na mke huyu wenye furaha asubuhi ya leo wanapokuja na sehemu hii ya furaha ambayo umeongezea kwenye ndoa yao, mtoto Samuel Thomas, Baba Mungu, tunaomba ya kwamba utambariki mtoto huyu. Na tunapomwinua Mbele Zako asubuhi ya leo, Bwana, kusudi mikono Yako mitakatifu isiyoonekana imbariki mtoto huyu. Na iwe hivyo, Bwana, kwamba mtoto huyu ataishi. Na endapo kuna kesho, jalia awe mfanya kazi hodari kwa Ufalme wa Mungu. Wabariki wazazi wake. Na sasa, Baba, tunakupa Wewe mtoto Samuel Thomas, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya maisha yaliyowekwa wakfu kwa Ufalme wa Mungu. Amina.

¹⁸ Mungu akubariki pamoja na mumeo, na uwe na furaha. Na iwepo sehemu ndogo inayoangaza maishani mwako, kote katika safari yako. Mungu akubariki.

¹⁹ Sasa, je! huyu ndiye mtoto anayehusika? [Mama yake anasema, “Ndiyo,” halafu mtoto anatoa sauti—Mh.] Sasa, siwezi kuielewa lugha hiyo. Ninajua kitu gani. Ninajua kile—kile wanachofanya, bali siifahamu.

²⁰ Nilipokuwa Ujerumani si muda mrefu uliopita, nisingeweza kuzungumza neno moja. Nilisema, “Lakini jambo, kuwahusu ninyi Wajerumani hapa,” nikasema, “sielewi.” Nikasema, “Kila... Nilikuwa nikienda zangu mtaani, na mama mmoja alikuwa amembeba mtoto mchanga, naye alikuwa akilia katika Kiingereza.”

²¹ Vema, ninaamini anapaswa kufanya jambo fulani. Nitakuwa nimewanyonganyonga kabisa ninyi nyote, tutakapofika kwa Meda. Wananyongwanyongwa sana katika kitu hiki, mnajua, kubanwa sana. [Mama huyo anasema, “Alicia Kay.”] Alicia Kay. [Mtu fulani anasema, “Carlyle.”] Carlyle. Alicia Kay Carlyle, hilo ni jina la kupendeza. Ninalipenda hilo. Waweza kumleta huyo dada mdogo hapa? Hum! Loo, hivi nimeushika mkono wako humo, pia, dada?

²² Vema, mwajua, wakati Israeli walipoleta dhabihu yao (ambalo nililithubiri jana) madhabahuni, mnaona, wangeweka mikono yao juu yake, kwa kuwa walijitambulisha wenyewe na dhabihu yao.

23 Mikono yako ikiwa juu ya mtoto wako, inakutambulisha na mtoto huyo basi. Hilo ni sawa? Nasi tunaweka mikono yetu juu yake, tukijitambulisha wenyewe katika maombi kwa Mungu, kwa ajili ya mtoto huyu Alicia Kay. Hilo ni sahihi? Carlyle.

24 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuinulia, maskini msichana huyu, Mungu, kipenzi hiki cha furaha ambacho kimepewa familia hii. Mbariki msichana huyu mdogo, Bwana, kitu hiki kidogo kirembo ninachokishika hapa mikononi mwangu asubuhi ya leo, wakati mama huyu anapomleta mtoto huyu mchanga. Ulimpa yeye, na sasa yeye anakurudishia Wewe. Inaonyesha imani yake na shauku, Bwana, kwamba mtoto wake atalelewa katika maonyo ya Mungu. Mbariki, Bwana, na jalia aishi maisha marefu yenye furaha, na awe mtumishi Wako mkuu katika mambo ya kesho, endapo kuna kesho. Bariiki makazi anamotoka. Tujalie, Bwana. Sasa, tunakupa Wewe msichana huyu mdogo mrembo katika kuwekwa wakfu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

25 Sasa, hivi huyo si ni mtoto mrembo sana. Mwajua, kila mtoto mchanga wa mama ndiye aliye mrembo sana ulimwenguni. Hiyo ni kweli, siyo? Mungu akubariki, maskini mtoto wa kupendeza sana. Ananiangalia, huku namna hiyo. Sasa nimeupinda mkono *wangu*.

26 Sasa, u hali gani? Vema, ni msichana mdogo mrembo jinsi gani huyu alivyo, pia. Jina lake ni nani? [Mama yake anasema, "Letha Ann Farmer."—Mh.] Letha, Letha Ann. ["Letha."] Letha Ann Farmer. Jamani, ni msichana mdogo mrembo jinsi gani! Waweza kuja hapa, uwe pamoja nami? Unaona? Hilo linapendeza. Sasa, huyo ni msichana mdogo mrembo, pia. Anaonekana ni mzuri, pia. Je! unapenda kwenda kanisani, Letha? Sasa, ningewazia, jamaa wadogo kama hawa ambao Bwana wetu aliwachukua mikononi Mwake. Hawa akina dada? ["Naam."] Mwajua, nimesimama hapa sasa, jinsi ninavyohisi hilo. Mnaona ninalomaanisha? Ni ndoa ya jinsi gani ama ni kuwekwa wakfu kwa jinsi gani? Unasimama kwenye njia ya Mungu. Loo, jamani! Linanitetemesha.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

27 Ee Mungu, tunakuja asubuhi ya leo pamoja na mtoto huyu Letha. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utambariki Letha na yote afanyayo kote maishani. Jalia aishi maisha marefu, yenye furaha. Wabariki wazazi wake. Jalia alelewe nyumbani, Bwana, apate kumpenda na kumwabudu Mungu. Na ninaomba ya kwamba kukiweko na kesho, kutakuwako, atakuwa ni mfanya kazi katika Ufalme wa Mungu. Yaweke magonjwa na kadhalika mbali naye wakati akisafiri. Na umfanye baraka kuu katika Ufalme Wako. Na tunakupa Wewe msichana huyu mdogo katika kuwekwa wakfu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mtoto wa kupendeza sana!

²⁸ Loo, ninawapenda watoto wadogo. Lakini ninaninii tu... Sikuzote nahofu kwamba watavunjika, mwajua. Wao ni wadogo tu sana. Na hata hivyo, mke wangu aliniambia, kasema, “Mbona, wangukuwa ni wagumu kuvunja kuliko—kuliko—kuliko ningalikuwa.” Kwa hiyo, naam, hiyo ni kweli. Wao ni wepesi sana, mwajua.

²⁹ Na sasa, je! kuna mtu aliye mgonjwa ambaye alitaka kuombewa, haja tu ma—maalum ya kuombewa ama chochote kile, nasi tungekuombea? Vema, dada, kama ungeweza kuja papa hapa na kusimama. Vema. A-ha. Hiyo ni... Tunataka kuyafanya mambo haya, ili kwamba mkishikwa sana na ujumbe wetu wa Krismasi, hiyo itakuwa ni sawa. Vema, bwana.

³⁰ Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Ndugu Neville, ungeweza kuja mbele pamoja nami?

³¹ Baba yetu wa Mbinguni, kwenye mkesha huu wa Krismasi, ambapo lile ondoleo kuu la dhambi zetu na maradhi lilizaliwa ulimwenguni, lipate kuwa Dhabihu kwa ajili yetu. Tunamleta dada yetu, katika Jina la Yesu Kristo, kwamba, tukiweka mikono yetu juu yake, kufanya kile hasa ulichosema tufanye. “Kuweka mikono juu ya wagonjwa nao watapata afya.” Tunafanya jambo hili katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya kuponywa kwake. Amina.

³² [Ndugu Branham anazungumza na mtu fulani—Mh.] Mpigie simu Ndugu Cauble...?...

³³ Loo, hiyo ni kweli? U hali gani, dada? Sasa, sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu tena.

³⁴ Baba yetu wa Mbinguni, tunaposimama hapa mbele ya Mwenyezi, tukimwomba dada yetu ambaye amepatwa na msiba. Na kuna jambo lililofanywa ambalo lililitia tu upofu jicho lake. Lakini Wewe, Bwana, kama ulivyomwambia Musa, “Ni nani anayeumba jicho la mwanadamu?” Na kuna mmoja tu anayeweza kusaidia, na huyo ni yule Yehova mkuu, Muumba. Kwa hiyo tunaomba, Baba wa Mbinguni, kama tunavyoamini hili miyoni mwetu, nasi tunamleta Kwako. Na imani yetu, tu—tunakuja kwa imani, huko kwenye madhabahu kuu ya thamani kuu ya Mungu, ambapo ile Dhabihu iliyojaa damu, Kristo, imewekwa madhabahuni. Na katika Kitabu cha Isaya, mlango wa 53 na kifungu cha 5, ilisema, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumeponywa.” Sasa tunaiweka imani yetu pamoja na yake, juu ya madhabahu Yako, na kuomba, katika Jina la Yesu, ya kwamba upofu huu utamwacha dada yetu, na ya kwamba ataweza kuona, kwa heshima na utukufu wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, dada.

³⁵ Ndugu Cauble. [Ndugu Wallace Cauble anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Paris Reidhead. Naam. Naam, bwana. Vema.

³⁶ Sasa tunaomba upako kwa ajili ya huduma ya Ndugu yetu Cauble, aende akamtembelee rafiki yangu. Nilifanya kazi pamoja naye huko New York. Paris Reidhead, yule aliyekuja nyumbani kwangu kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.

³⁷ Na je! hivi hakuwa na ushusiano na Misheni ya Sudan? [Ndugu Cauble anasema, “Naam. Yeye ni mkurugenzi wa Afrika nzima. Anaishi New York, katika sehemu ya New York pale, akifanya kazi kwenye kanisa hili kubwa pale, kusaidia.”—Mh.] Ajabu sana. Basi unahama Louisville. [“Naam.”] Loo, jamani! Tunachukia kupungukiwa na Ndugu Cauble, kuondoka Louisville. Nakutakia heri, ndugu. Jamani!

³⁸ Daima ningemkumbuka Ndugu Cauble. Ndugu huyu wa thamani, mtakatifu wa Mungu, ninakumbuka nilipokutana naye kwa mara ya kwanza. Alikuwa akitokwa na damu karibu na kufa. Ni—nilijua jina lake mashuhuri miongoni mwa ndugu. Nilienda kule. Kulikuwako na ndugu waliokuwa wamesimama hapa hospitalini. Mimi, maskini jamaa mdogo kama mimi, niliona haya kuingia, kwa hiyo nikapiga magoti nyuma ya kitu cha Coca Cola nje katika ukumbi wa hospitali hiyo na kumwombea kisha nikarudi.

³⁹ Simu ikalia tena, ikasema, “Hujakuja kamwe kumwona Ndugu Cauble.”

⁴⁰ Ndipo nikaenda kule. Walikuwa wamekifanyia kitu fulani upasuaji puani mwake, na kukata, wakakatilia mbali kitu fulani, naye alikuwa akitokwa na damu sana. Nikapiga magoti hapo nikaomba. Ikakoma mara moja.

⁴¹ Baba yetu wa Mbinguni, yeye ni mtumishi Wako. Na sasa anaondoka miongoni mwetu, lakini tungali tumeungana, Bwana. Mioyo yetu daima itadunda, naomba, kama inavyounda sasa, mmoja kwa mwingine. Ninakuomba, Baba, umbariki huyu, ndugu yangu, wakati akienda kumsaidia yule mtumishi Wako mashuhuri, Ndugu Paris Reidhead, akiwa ana shauku sana ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Haidhuru ni kitu gani wa kimsingi wote wanasema, yeye angali anamtaka Mungu, kwa vyovyote vile. Mbariki Ndugu Cauble, na uwabariki pamoja katika kazi yao kwa ajili Yako, Bwana, juhudi zao. Jalia wafanye kazi kwa ushirikiano, kama vile Paulo na Sila. Tujalie, Bwana.

⁴² Mpe upako wa Roho Mtakatifu. Amekuwa na shauku sana, na amejaribu, na kung’ang’ana, na kusukuma, kupatafuta mahali pale ambapo Wewe ungeweza kweli kumjaza, Bwana, na kumfungulia mambo makuu. Basi jalia huu uwe ndio ule wakati, Bwana, ambao ulimfunza na tukaomba kwa wakati huu, Bwana, kwa maana tuko katika wakati wa jioni. Upe mwili wake nguvu, Bwana. Anahitaji nguvu. Jalia nguvu zilizomfufua Yesu

Kristo kutoka kwa wafu, zilete uponyaji mwilini mwake, nguvu za kubadilisha, jalia aende hivyo katika nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo. Tunambariki.

⁴³ Bwana akubariki, Ndugu Cauble! Msalimie Ndugu Paris kwa niaba yangu, nami nitatumaini kuwaona nyote baadaye. Ninaenda ng'ambo, India. Mungu akubariki.

U hali gani, dada? Asante, ndugu.

⁴⁴ Bwana Yesu, tunapomleta msichana huyu, huku mikono yetu imewekwa juu yake, tukijiunganisha wenyewe kwake, kama vile kwa dhabihu, tukijua ya kwamba Wewe uliahidi hilo, naomba kwa ajili ya uponyaji wake katika Jina la Yesu. Amina.

⁴⁵ Kwa maskini mama huyu anayesimama hapa akiwa na bega lililoinama na nywele zenye mvi, akionyesha ya kwamba amepambwa kwa ajili ya ulimwengu ujao. Mungu, jalia nguvu zilizomfufua Bwana wetu Yesu kutoka kaburini, tunapoweka mikono yetu juu yake, tukijiunganisha pamoja naye na Kristo, jalia nguvu zilizomfufua kutoka kaburini ziuponye mwili wake, katika Jina la Yesu.

Mungu akubariki, dada yangu.

⁴⁶ Baba wa Mbinguni, tunapoweka mikono yetu juu ya dada yetu, vivyo hivyo, katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe kwa utukufu wa Mungu. Amina.

⁴⁷ Baba wa neema, katika Jina la Yesu Kristo, tunaweka mikono juu ya dada yetu. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe kwa utukufu wa Mungu. Amina.

Mungu akubariki, dada.

⁴⁸ Baba wa Mbinguni, tunaweka mikono yetu juu ya ndugu yetu hapa, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake. Jalia aponywe katika Jina la Yesu.

⁴⁹ Baba yetu wa Mbinguni, kwa kuwa mmoja wa dada zetu husafiri mbali, apate kuwa mkutanoni, lakini amesimama asubuhi ya leo, nasi tunajiunganisha pamoja, Bwana, katika Injili, huku tumewekeana mikono yetu mmoja juu ya mwingine na juu yake. Jalia Mungu wa Mbinguni aone jambo hili, mahali linaposema, "Wakiwepo wawili ama watatu watakaokubaliana juu ya nchi." Sisi hapa tumesimama, watatu pamoja, Bwana, katika Jina la Yesu Kristo. Mponye, Bwana, katika Jina la Yesu.

⁵⁰ Vivyo hivyo, Bwana, tunaweka mikono yetu juu ya dada yetu hapa. Na vile tunakubali, katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

⁵¹ Baba wa Mbinguni, kasema maisha yake ya Kikristo yaliyo mema sana . . . mke wake ana kansa. Ee Mungu, yeye anasimama kwa niaba yake. Kristo anasimama kwa niaba yake.

Sasa, ewe ibilisi, mwache, katika Jina la Yesu Kristo.

52 Amini jambo hilo, ndugu. Hii ni nguzo iliyoshindiliwa papa hapa. Ikumbuke siku hii.

53 Baba yetu wa Mbinguni, huyu ni dada yetu anayekuja kwetu, Bwana. Na kama maisha ya kielelezo, yeye anaishi, na anakuja kwa ajili ya uponyaji wake. Na sisi tukiwa na mioyo na mikono yetu imeunganishwa na Wewe, Bwana, tunaomba baraka hii, katika Jina la Yesu Kristo.

54 Dada yetu Risert, Bwana, ambaye ni mjakazi Wako, amekuja katika wakati huu wa Krismasi. Katika Jina la Yesu, jalia aponywe. Amina.

55 Baba wa Mbinguni, tunamleta maskini mwanamke huyu mzuri sana asubuhi ya leo, katika Jina la Bwana Yesu. Tunaweka mikono yetu juu yake na kuomba kwa ajili ya uponyaji wake, katika Jina la Yesu. Amina.

56 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja na kuweka mikono yetu juu ya dada yetu, katika Jina, lile Jina lililo takatifu kuliko majina yote, Yesu Kristo. Jalia aponywe kwa utukufu wa Mungu.

57 Baba yetu wa Mbinguni, tunapomleta Dada yetu Kwako leo, nya—nyara ya neema Yako, jinsi ambavyo umekuwa kwa mwanamke huyu. Miaka na miaka iliyopita, akiwa tu na saa chache za kuishi, ameliwa na kansa, naye ameuishia Ufalme wa Mungu. Mponye leo, Bwana, kutokana na athari ya maradhi yoyote, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki.

58 Baba yetu wa Mbinguni, wakati dada yetu, pia kumbukumbu ya neema ya Mungu, pia. Maskini mwenye mashaka na mtumwa wa dawa za kulevya, mlevi, na sasa anasimama mwanamke wa kupendeza aliyeponywa. Ni kisa cha uponyaji cha jinsi gani, Bwana! Na kisha moyo wake unauma kwa ajili ya wengine wanaoteseka, kwa sababu anajua kuna Mponyaji mkuu. Alitamka majina matatu mbalimbali sasa hivi, Baba. Naomba na kujiunganisha mwenyewe pamoja na ndugu yetu hapa, mchungaji wetu, na—na dada yetu, na Bwana Yesu. Na jalia, katika Jina Lake tukufu, watu hawa watatu wakombolewe kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Amina.

Asante, ndugu.

59 Baba mtukufu, tunaweka mikono yetu sasa juu ya Ndugu yetu Way. Yeye anaomba mambo matatu. Wewe unayajua, Bwana. Na tunaamini ya kwamba imeandikwa, na tunajua ya kwamba Maandiko yanasema, “Mambo yote.” Na kwa hiyo tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba hili, aliloomba, litadhihirishwa kwake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

60 Baba mtukufu, tunaweka mikono juu ya ndugu yetu, katika Jina la Bwana Yesu, na kuomba kwa ajili ya uponyaji wake, kwa utukufu wa Mungu. Tujalie hilo, Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

61 Baba wa Mbinguni, juu ya dada yetu, tunaiweka mikono yetu, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, kutii yale aliyosema tufanye. Jalia aponywe katika Jina la Yesu. Amina.

Ubarikiwe, dada.

62 Baba Mungu, vivyo hivyo, juu ya ndugu yetu, tunaweka mikono yetu, katika Jina la Yesu Kristo, kwamba umpe afya, kwa ajili ya ufalme wa Mungu. Amina.

Mungu akubariki, ndugu yangu.

Dada Arganbright.

63 Baba wa Mbinguni, tunamwomba Dada Arganbright, kwamba Wewe utamponya. Tujalie hilo, Bwana. Ombi lake, na ajaliwe, Baba yetu wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

64 Bwana Yesu, tukiweka mikono juu ya ndugu yetu, katika Jina la Yesu Kristo, jalia ombi lake litimizwe. Amina.

Amini hilo, ndugu yangu.

65 Baba wa Mbinguni, tunaweka mikono yetu juu ya mvulana huyu mdogo, katika Jina la Yesu Kristo, na jalia, tunaposimama pamoja asubuhi hii, kwa imani, tunamleta mtoto huyu Kwako. Basi jalia baraka za Mungu, nguvu za uponyaji za Kristo, na zidhihirishwe katika mwili wake mdogo, katika Jina la Yesu. Amina.

66 Baba Mungu, juu ya baba huyu mpendwa anayemleta, tunaomba pia ya kwamba utadhihirisha nguvu Zako za uponyaji, katika Jina la Yesu. Amina.

Ubarikiwe, ndugu yangu.

67 Baba wa Mbinguni, wakati Dada Peckenpaugh, dada yetu mwadilifu aliye na haja, na jinsi umekuwa mwenye neema kwake, Bwana. Ninaomba ya kwamba mwendeleo Wako wa baraka utiririke moyoni mwake. Na magonjwa yote na huzuni ambazo amepitia, jalia nguvu za Kristo zimrejee, Bwana, mara mia moja, na umpe afya kabisa, wapendwa wake, katika Jina la Yesu. Amina.

Ubarikiwe.

68 Baba wa Mbinguni, tunaweka mikono juu ya ndugu yetu na kuomba ya kwamba nguvu za Yesu Kristo zimponye, kwa Jina la Huyu Mtoto-Kristo ambaye tunamsherehekea wakati huu. Amina.

69 Mungu mwenye neema, tunapomwekea dada yetu mikono, mjakazi wako, katika Jina la Yesu Kristo jalia aponywe kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

70 Bwana, tunaweka mikono juu ya dada yetu, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia aponywe. Amina.

⁷¹ Baba wa Mbinguni, tunaweka mikono juu ya dada yetu hapa, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia nguvu za Mungu zimfanye aponywe. Amina.

⁷² Bwana Yesu, mjalie dada yetu ombi lake, tunapoomba kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu. Amina.

⁷³ Baba yetu wa Mbinguni, tunamwona maskini dada yetu angali yu pamoja nasi, miaka hii yote. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hilo, Bwana. Tunaomba ya kwamba utamjalia ombi lake, katika Jina la Yesu.

Bwana Mungu . . .

⁷⁴ Ati nini? [Huyo dada anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Na Mungu yupo kila mahali, baharini kote hapa, kila mahali. Nawe unaamini, na Mungu ataninii, asubuhi ya leo, huko Norway, atamponya? [Dada huyo anazungumza na Ndugu Branham.] Ati nini? Binti yako na baba yako, na unataka waombewe, wokovu.

⁷⁵ Bwana, unamwona maskini mama huyu nasi tunajua ya kwamba Wewe unajua maombi yake. Uliisikia sauti yake. Unajua je yeye amesimama hapa? Wakati, si hata shomoro anaweza kuanguka mtaani bila ya Wewe kujua. Na tena basi najua ya kwamba Wewe unajua ombi hili, kwa hiyo tunayataja tu mambo haya, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia apewe, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

⁷⁶ Baba wa Mbinguni, tunaomba ya kwamba, kwa ajili ya mama yake ambaye ni mzee na anaenda kufanyiwa upasuaji. Mungu, msaidie. Na endapo kuna jambo lingine zaidi tunaloweza kufanya, Bwana, linene kwangu tu ama kwa mtu fulani, kabla ya siku hii, kumfariji ndugu yetu. Tujalie, Baba. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁷⁷ Bwana, tunaweka mikono juu ya dada yetu. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba umponye na umpe afya. Amina.

⁷⁸ [Dada mmoja anasema, “Ndugu Branham, ninataka kusimama. Ninataka uje . . . ? . . .”—Mh.]

Mungu wa Mbinguni naomba umjalie ombi lake. Katika Jina la Yesu, naomba.

Mungu akubariki, dada. Wewe ni Dada Margaret. Naam. Vema.

⁷⁹ Bwana Yesu, ninamwomba dada ye—yetu, mumewe anasimama kwa niaba yake. Jinsi wanavyojitahidi, na jinsi Wewe umejidhihirisha kwao na kujionyesha kwao, Mungu! Ninashukuru sana. Jalia, Bwana, ya kwamba mke wake ataponywa, dada yetu wa thamani, katika Jina la Yesu.

⁸⁰ Baba wa Mbinguni, ombi hili ambalo ndugu huyu anaomba, Wewe unajua yote kuhusu hali hizi, Bwana. Ninamwomba mtumishi Wako. Mungu, tujalie, na kwa uponyaji wa miili ambayo ananena habari zake. Sasa, umeyasikia maombi hayo

vizuri kuliko nilivyoyasikia. Kwa hiyo ninaomba tu, moyo wangu ukiwa wazi, juu ya madhabahu Yako, na ninaweka ombi langu pamoja na la ndugu yangu hapa, katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba yatajihiwa. Amina.

⁸¹ Baba wa Mbinguni, tunaweka mikono juu ya dada yetu kwa ajili ya ombi lake. Jalia atimiziwe katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, dada.

⁸² Bwana, tunaweka mikono juu ya dada yetu, kwa ajili ya ombi lake. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia lijibiwe.

⁸³ Baba Mungu, juu ya ndugu yetu hapa, ombi lake, ajibiwe, Bwana. Yeye amejaribu kukutumikia, miaka hii yote. Kupitia hali ngumu, angali anasimama moja kwa moja. Mungu, jalia aushike upembe wa madhabahu asubuhi ya leo, apigilie kigingi hapa kando yake, “Hii ndiyo saa utakapokuja.” Tujalie. Na jalia ombi hili lijibiwe kwa ajili ya mkewe na mjukuu wake, katika Jina la Yesu.

Mungu akubariki, Ndugu Brewster. Amini hilo.

⁸⁴ Baba yetu wa Mbinguni, maskini mama huyu, ambaye amesimama hapa asubuhi ya leo, amekuwa kama mama kwa wengi. Sasa anaomba kwa ajili ya wapendwa wake, Bwana. Ameomba hilo, nasi tunaninii... tunaweza kujiunga sote pamoja, tukiweka mikono yetu juu yake, kama kitu kimoja, kwamba tunaamini hili. Na huku mioyo yetu ikiwa mbele ya madhabahu Yako, tunaomba kwa ajili ya haja hii ambayo anaomba, ajaliwe katika Jina la Yesu. Amina!

⁸⁵ Mungu, Wewe unawajua watu anaowasimamia, kila mmoja aliye moyoni mwake wakati huu. Nasi tumejiweka pamoja naye, Bwana. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia haja yake itimizwe. Amina.

⁸⁶ Ee Mungu, tunamfahamu Dada Hattie. Tunaomba, Mungu, tunapoweka mikono yetu juu yake, jalia kwamba Roho Mtakatifu atakuwa pamoja naye, na afunulie moyo wake tena. Tunawazia juu ya wavulana wake wa thamani, wote wawili. Ninawaza juu ya kuketi pale kwenye kile chumba siku ile, katika nyumba ndogo, duni. Wewe ukasema, “Mwambie aombe chochote atakacho, kisha useme tu Neno.” Akaomba. Mungu, ninajua ya kwamba unawajali watu hawa. Kwa hiyo ninaomba, ninapomwekea mikono, katika Jina la Yesu Kristo, ombi lake na lijibiwe.

⁸⁷ Bwana Mungu, tunapoweka mikono juu ya maskini dada yetu, akiendesha kwenye barabara hizi zinazoteleza na kadhalika, akijaribu kufika hapa. Unajua yote kuhusu jambo hilo. Ninamwomba, Bwana, ninapoweka mikono yangu juu yake. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia apokee kile alichoomba. Amina.

⁸⁸ Baba yetu wa Mbinguni, wakati ndugu huyu wa thamani . . . jinsi ambavyo aliyakinia wakati mmoja, Bwana, maskini sigara hizo na kadhalika zilikuwa zimemfunga. Angepata mazungumzo ya faragha mara moja, na angengojea na kungojea. Wala usingetwambia kitu. Angepata mwingine. Mtu ungengojea na kungojea, wala usingetwambia kitu. Na hatimaye, asubuhi moja, tulipokuwa tumeketi pale, hili hapa likaja. Yote yalikuwa yamekwisha basi. Tunakushukuru, Bwana. Wewe ni wa kweli. Maneno Yako hayashindwi kamwe. Naye alisema, “Wale wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya.” Sasa, yeye anakuja na haja tatu asubuhi ya leo, Bwana. Nasi tunasimama kama watatu, kukiweko na ahadi ya o—ofisi ya utatu iliyofanywa katika Mungu mmoja. Katika Jina la huyo Mungu mmoja wa kweli, aliye hai, Yesu Kristo, jalia ombi lake litimizwe kwake. Amina.

Mungu akubariki, ndugu.

Bwana . . .

Loo, jamani! [Dada mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.]

⁸⁹ Bwana, unasikia maombi hayo. Wewe unajua jinsi ya kuyajibu, Bwana. Kwa hiyo tunaweka tu mikono juu ya Dada yetu Baker, katika Jina la Yesu Kristo, tunatoa maombi yetu pamoja na yake, kwa ajili ya uponyaji. Amina.

Ubarikiwe, dada yangu.

⁹⁰ [Ndugu Neville anasema, “Mtu yeyote anayeingia, na aingie sasa.”—Mh.]

⁹¹ Baba wa Mbinguni, ninapomwekea mikono ndugu huyu mzuri, inaonekana kama picha halisi ya afya leo, bali wakati mwingine hilo linadanganya. Kwa hiyo ninaomba ya kwamba utamjibu ombi lake, chochote kilicho moyoni mwake. Mpe alichoomba, katika Jina la Yesu. Amina.

⁹² Baba wa Mbinguni, tunaweka mikono juu ya dada yetu na kuomba ya kwamba, katika Jina la Bwana Yesu, kwamba utamkirimia ombi lake kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

⁹³ Bwana Yesu, tunaweka mikono juu ya ndugu yetu na kuomba kwa ajili ya ombi lake. Tunaonyesha tu jambo hili, Bwana, tunapoweka mikono juu yake. Tunaungana pamoja, na katika umoja huu tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki, ndugu yangu.

⁹⁴ Baba Mungu, kwa dada yetu pia, tulifanya vivyo hivyo. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia apate haja yake.

Ubarikiwe, dada yangu.

⁹⁵ Mungu, kama vile ambavyo ndugu yetu wa thamani angeliweza kuuawa hivi majuzi, ila Wewe hukuwa tayari kwake.

Kwa hiyo ninaomba, Mungu, kwamba utampa ombi lake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Unajua jinsi ya kuamini jambo hilo.

⁹⁶ Baba yetu wa Mbinguni, wakati maskini dada yetu, mwenye wasiwasi anapokuja huku mbele, ukijua, Bwana, ya kwamba mateso yake yamekuwa ni mengi. Bali Wewe umeahidi ya kwamba, “Mateso ya mwenye haki ni mengi, lakini Mungu atamponya nayo yote.” Yeye anahitaji sana ukombozi huu, Bwana. Tunaweka mikono juu yake na kulaani uovu huu. Bwana, juu ya madhahabu Yako ya dhahabu, jalia nguvu za Mungu zimgharikie na kumpa afya. Amina.

⁹⁷ Vema. Nyote mtabaki. Je! wewe ulikuwa umeketi huko nyuma wakati wote? Naam. Sikukuona. Loo, wewe, upande *huu*. Si ajabu. Huyu ni mtu ambaye anaitwa, wanamwita, “Miner”. Hilo ndilo jina lake. Ila huu ndio wakati mmoja ambapo hilo Miner ni major. [Ndugu Miner Arganbright anasema, “Ati niseme nini?”—Mh.] Sema chochote, chochote utakacho.

⁹⁸ Ndugu Miner Arganbright ni mmoja wa Wa—Wafanya Baiashara wa Full Gospel, mmoja wa ninii... alisaidia kuanzisha shirika hili kuu, ambalo tunajaribu kufanya kazi pamoja kuwafanya watu wote watambue, pasipo kujali uanachama wao na dhehebu lao, ya kwamba sisi sote ni ndugu katika Kristo.

⁹⁹ Yeye alisema jambo fulani dogo, hivi majuzi. Alimwandikia Seneta ama mtu fulani huko juu. Kilikuwa ni kitu adhimu sana. Nami nikasema, “Ninataka uliandike. Ninataka ushuke uje kanisani na kusema jambo hili.”

Kasema, “Tayari nimelisema.”

Kwa hiyo tunalo hapa kwenye kanda. Na ninataka hayo yatolewe kwenye kanda, ninyi ndugu. Ndugu Jim, ninajua unanisikiliza hapo ndani, chumbani. Ninataka hilo. Hiyo kweli ilikuwa ni sehemu halisi ya—ya diplomasia, iliyoongezewa mle. Mnaona? Vema.

¹⁰⁰ Sema unalotaka kusema, Ndugu Arganbright. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Amina. Amina.

¹⁰¹ [Ndugu Arganbright anasema, “Hebu nikae pale. Hilo ni sawa, pale pale.”—Mh.]

¹⁰² Ni kweli jinsi gani! Amina. Ni kweli jinsi gani! Amani huja na kwenda, na anasa, na inafifia tu, bali furaha inadumu.

¹⁰³ Vema, ni ninii—ni ninii—siku mbaya huko nje, siku nzuri ndani. Na, mwajua, nilikutana na mtu fulani, ama mtu aliyeniambia kuhusu kukutana na mtu mmoja hivi majuzi, naye alisema alikuwa akinung'unika. “Loo,” kasema, “hii ni siku mbaya sana.” Alisema ilikuwa ikinyesha na kuendelea.

Akasema, “Hii ni siku nzuri sana.”

104 Ndipo jamaa huyo akasema, “Vema, unawezaje kuiita hii ati ni siku nzuri sana?”

105 Akasema, “Nitakwambia. Daktari aliniambia mwaka mmoja uliopita nilikuwa tu na juma moja la kuishi.” Kasema, “Kila siku, vema, hiyo ni siku nzuri sana.” Naam.

106 Kwa hiyo hilo ni kweli, ni—ni siku nzuri sana, kwa hiyo sisi sote tunaninii...Kile ninii...kama ndugu alivyosema, “Sisi sote tulihukumikiwa kifo.” Hiyo ni kweli, kufa na kwenda matesoni. Lakini sasa hii ni siku nzuri sana. Sisi tu hai katika Kristo wala hatuwezi kufa tena. Yote yamekwisha, mnaona. Kweli sisi tumo katika Kristo. Sasa hebu tuninii...

107 Sasa, kwenye maskani, Ndugu Arganbright, kwa kawaida mimi huchukua tu wakati wangu. Kwa hiyo ukiona njaa inapokaribia chakula cha jioni, unaweza kuponyoka... Ninajisikia kuchoka sana asubuhi ya leo ilinibidi tu niseme jambo fulani kusudi nipate nguvu kidogo mpaka ninapoweza... Roho wa Mungu aje juu yangu.

108 Kwa hiyo hebu na tuinamisha vichwa vyetu sasa na kuomba kabla hatujalisoma Neno. Ni maombi mangapi kwa ajili ya mambo mengine mliyo nayo ambayo labda hamkuombewa, hebu tu na yajulikane mnapoinua mikono yenu. Sasa hebu—hebu tusimame asubuhi ya leo tunapoomba. Hiyo itakupa nafasi ya mkao na labda itasaidia kidogo. Halafu baada ya maombi, ninawatakeni mwendelee kusimama kwa dakika chache tu mpaka nitakapolisoma Neno. Nafikiri hilo ni jambo zuri sana kusimama kwa uchaji tunapolisoma Neno la Mungu.

109 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja tukiwa wanyenyekevu tu kadiri tujuavyo jinsi ya kuja, tukiwa na mioyo iliyoondolewa tamaa zote za ulimwengu ama anasa zake. Na kama vile ndugu yetu amenukuu ama kutwambia, “Furaha, furaha ya Bwana ni nguvu zetu.” Nasi tunakuja tukiwa na mioyo yenye furaha, kwamba tuna majaliwa haya ya kuja katika Uwepo Wako, kuomba haja yoyote ambayo tungetamani. Na furaha huja tunapoangalia katika Neno. Na tumeahidiwa kama tungeliamini, tungepewa haja hiyo. Ni kitu gani kingeliufurahisha sana moyo wa mwanadamu unaodunda-dunda, zaidi kuliko kujua ya kwamba Mungu wa Milele, asiyeapatikana na mauti alitoa ahadi kama hiyo?

110 Sasa tusamehe, Bwana. Na iwapo tumetenda dhambi ama tukafanya jambo lolote ambalo halikukufurahisha, kwamba kabla hatujaomba mambo haya...Kwa kuwa tunajua kwamba imeandikwa, “Mioyo yetu isipotuhukumu, tumepata haja yetu.” Lakini sasa tusamehe yote hayo tuliyofanya. Tuangalie, Bwana, kwa rehema na kwa huruma. Angalia jinsi tulivyo kundi la kusikitisha, Bwana. Maskini wanadamu, tukitambaa huku na huko humu duniani, na tukijikokota tu kupitia mahali hapa penye dhambi, bali ndani katika kilindi cha moyo wetu

tunajua ya kwamba kuna Mtu anayekuja siku moja ambaye atatuinua kutoka mahali hapa atupeleke mahali pazuri zaidi, nasi tunafurahi katika jambo hili.

¹¹¹ Nami ninaomba, Mungu, kwa ajili ya kila haja. Ulijua kile kilichokuwa nyuma ya mikono hiyo iliyoinuliwa. Wajalie, Bwana. Ninajiombea mwenyewe, kwa ajili ya nguvu asubuhi ya leo, kwa—kwa ajili ya sauti ya kunisaidia na kuihubiri Injili. Na sisi tungeomba ya kwamba ungetubariki pamoja katika jambo hili tungalosherehekea, msimu wa Krismasi. Bwana, jalia tupate Roho halisi ya Krismasi, na jalia ikae pamoja nasi milele. Kwa kuwa tunaomba jambo hili katika Jina la Yesu na kwa ajili Yake. Amina.

¹¹² Sasa, kama mtasimama tu kwa dakika moja, ninataka kusoma asubuhi ya leo kutoka katika Kitabu cha Mika, mahali pamoja; na mahali pengine, kutoka kwa Waebrania, mlango wa 12 wa Waebrania, kwa ajili ya ninii... kukusanya muktadha mdogo wa yale ningetaka kuzungumzia asubuhi ya leo kwa ajili ya ujumbe wetu wa Krismasi. Ni, Waebrania 12:25. Kwa namna fulani ilinibidi kuharakisha asubuhi ya leo nilipoamka, wala sikuwa na kila kitu mahali nilipotaka kuwa nacho, nilipotaka kuwa napo, hasa. Ninaanza na kifungu cha 2 katika Mika 1.

Sikilizeni, . . . enyi watu; sikiliza, ee dunia, na vyote vilivyomo; Bwana MUNGU na ashuhudie juu yenu, yeye Bwana kutoka hekalu lake takatifu.

Kwa maana, angalieni, BWANA anakuja akitoka mahali pake, naye atashuka, na kupakanyaga mahali pa dunia. . .

Na hiyo milima itayeyuka chini yake, nayo mabonde yatapasuliwa, na kama vile nta iliyo mbele ya moto, kama maji yaliyomwagika tena kutelemka gengeneni.

¹¹³ Na katika Waebrania, mlango wa 12 na kifungu cha 25, tunasoma jambo hili.

Angalieni msimkatae yeye anenaye. Maana ikiwa hawakuokoka . . . Maana ikiwa hawakuokoka wale waliomkataa yeye aliyewaonya juu ya nchi, zaidi sana hatutaokoka sisi tukijiipusha na yeye atuonyaye kutoka mbinguni.

¹¹⁴ Sasa, Bwana Mungu, ongeza baraka Zako katika kusomwa kwa Neno Lako, na utupe kila mmoja leo ja—jambo ambalo ungetutaka tujue, tupate kuondoka hapa na kujisikia ya kwamba tumekuwa katika Uwepo Wako, na tunaweza kusonga mbele tukiwa na m—mtazamo mpya na ufahamu bora zaidi, na azimio bora zaidi ya tulilokuwa nalo tulipoingia kwenye jengo hili. Kwa kuwa tunaomba haya katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

¹¹⁵ Sasa, hapana shaka, kama ningelisikia kifungu hicho kikisomwa kwa ajili ya ujumbe wa Krismasi, ningelisema, “Sasa hilo si ni somo la kigeni la Krismasi?” Ninii... Kusudi langu katika kufanya jambo hili, lilikuwa ni kuliletea kanisa jambo fulani ambalo labda ni la tofauti kidogo, kwa sababu kote kwenye redio katika Krismasi mtakuwa mkisikia ile hadithi ya kale inayojulikana, tena na tena, juu ya wale mamajusi wakija kutoka Mashariki na kumpata mtoto Kristo, na kuabudu kwa wachungaji, na kule kutokea kwa ile Nyota, na hadithi hizi zote za Krismasi ambazo zinajumuisha imani yetu ya kidini ya siku hizi. Nazo zote ni nzuri sana, ni—ninashukuru kwa ajili ya jambo hilo. Lakini niliwazia kwenye kanisa asubuhi ya leo... Na labda mchungaji wetu, labda usiku wa leo ama Jumapili ijayo atakuwa analeta ujumbe wa kitu kama hicho. Basi nikawazia kuwapa watu ba—badiliko la mtazamo mwingine kutoka... kuhusu Krismasi, na mimi ningeninii... Nilichagua somo hili. Sasa, maneno machache tu.

¹¹⁶ Na sasa ninaona mnabadilishana mahali, wengine wanasimama, wengine wakiketi. Na hilo—hilo ni zuri. Na karibuni tutakuwa na nafasi kusudi tuninii... Hatuwezi, samahani hatuwezi kuyajaza marefu haya ya kanisa, kwa kuwa zimamoto wasingeturuhusu kufanya hivyo. Lakini tutaipanua kidogo hivi karibuni, Bwana akipenda. Tayari wameanza hilo, na—na hilo ni mara tutakapoweza tutapasimamisha, napo patakuwa ni mahali pa tofauti kabisa tuginena habari za nyenzo za mahali hapa. Kwa kweli hakutakuwako na kuonekana kwa ile maskani ya kale. Ni kwamba kutakuwako na madirisha yenye vioo vilivyotiwa rangi ya kuona, kutakuwako na matofali yaliyorembwa yaliyobandikwa yakiizunguka. Kutakuwako na... Itakuwa ni tofauti kabisa. Bali lile jengo la kale litabaki hapa, kwa maana tuna kusudi kwa ajili yake, mnaona. “Kuta za kale na zibaki,” mnaona. Nasi tutalifunika tu na kulizungushia mawe, na kadhalika, bali litabaki hata hivyo.

¹¹⁷ Sasa, Krismasi. Na—natamani kweli kwamba watu wangeninii, wangeweza kufahamu katika ulimwengu huu, kwamba Krismasi ni nini hasa. Sasa, neno la kwanza *Krismasi* ni ninii—kwa namna fulani ni tamshi la Kikatoliki. Linamaanisha “Ya Kristo...” *K-r-i-s-m-a-s-i*, mnaona, “Misa ya Kristo,” mnaona. Ilitengwa ama ilianzishwa na kanisa la Kirumi. Naye Kristo katu hakuzaliwa tarehe ishirini na tano Desemba zaidi ya nilivyojaliwa mimi. A-ha. Ni mkusanyiko mtupu kabisa wa fundisho la sharti. Hivyo tu. “Ulimwengu mzima,” kama nabii alivyosema, “umekuwa kidonda kitokacho usaha.” Hiyo ni kweli. Kabisa ni kwamba hakuna kitu kilicho safi popote. Kila sikukuu imeunganishwa na... Mbona, Baba Krismasi alipachukua mahali pa Krismasi, kule kuzaliwa katika hori. Sungura na kuku na kofia mpya zilichukua mahali pa ufufuo. Na Mungu anaonekana wapi katika haya yote? Mnaona? Sababu ya

jambo hili ni kwa sababu kwamba, mwanadamu, yuko kwenye biashara.

¹¹⁸ Mbona, walianza kununua zawadi za Krismasi miezi kadhaa iliyopita, na ni kitu gani ila tabia ya kikafiri! Hakuna kitu ambacho ni cha kiungu juu ya jambo hilo. Loo, wanajaribu kusema, “Kutoa zawadi, kwa mamajusi.” Hilo ni o—oasisi tu kwa udhuru wa ibilisi. Ukitaka kutoa kitu, ni maisha yako kwa Kristo. Msipeane mmoja kwa mwingine, mpeni Yeye. Hicho ndicho Yeye alifia. Hilo ndilo kusudi Lake la kuja. Mnaona?

¹¹⁹ Lakini imefikia mahali ambapo ni—ni—ni laana kwa watoto wadogo. Maskini jirani fulani huko chini mtaani anaweza kuwa na mengi, na maskini jamaa huyo mwingine hana kitu, nao wanaangalia. Na ni—ni kwamba kitu hicho chote ni kosa. Hivyo tu. Nao wafanya biashara wanaongeza bidhaa zao mahali hapa. Wao. . . Mbona, mke wangu aliingia kuwanunulia watoto fulani kitu fulani, na yapata majuma matatu yaliyopita, kasema, “Loo, tumeuza tukamaliza. Bidhaa zote. Tulifanya oda maradufu ya bidhaa mwaka huu, tayari tumeuza yote.” Majuma matatu ama manne kabla ya wakati wa kuanza kununua madukani. Loo, ni ujanja mkubwa wa kibiashara wa jinsi gani!

¹²⁰ Na, hata hivyo, je! mnajua jinsi Krismasi ilivyopata kuanza, hii ambayo tunaiita Krismasi, “Misa ya Kristo”? Hii hapa hadithi yake, mhitasari mdogo tu niliouandika hapa kwenye ukurasa. Ndio kwanza nimalizie mwaka jana, kabla sijakuwa na *Nyakati Saba Za Kanisa*, nilizifundisha hapa, nilichukua *Baraza la Nikea*, na *Kabla Ya Baraza La Nikea* na *Baada Ya Baraza La Nikea*, na *Wazee wa Nikea*, na *Babeli Mbili* kilichoandikwa na Hislop, na *Kitabu Cha Wafia Imani Cha Foxe*, na vyote, kwa sababu nimewasikia wahudumu wakikinukuu. Lakini nilitaka kukisoma mimi mwenyewe, kujionea, ili kwamba ni—ningejua ninapokisoma ama kuwaambia watu wangu, kwa sababu Mungu ataniwajibisha kwenye ile Siku ya Hukumu yale ninayowaambia watu. Kwa hiyo, sipaswi kusema kile mtu mwingine alichosema kwamba walisoma, ninataka kukisoma mimi mwenyewe, mnaona, na kujua.

¹²¹ Sasa, kwa kweli, Krismasi, Kristo, ninaamini na karibu ninaweza kuthibitisha. . . Kama vile ufufuo unavyoweza kuthibitishwa kwa kumwangualia Muumbaji, jinsi ambavyo aliumba mimea hii yote, na jinsi kila kitu kinachotumikia kusudi Lake hakina budi kufa, na, kikifa, kinaishi tena maana kina uhai wa kudumu. Lakini jinsi tu kinavyoweza kuishi tena, ni mbegu iliyorutubishwa. Mnaona? Sasa, Mungu hujidhihirisha katika uumbaji huo, na inaonyesha ya kwamba miungu hii yote ya kipagani na kadhalika tuliyo nayo si ya kweli. Mnaona, ni falsafa tu na mawazo. Lakini ninii—Yeye aliyeumba Mbingu na nchi anajidhihirisha kupitia maumbile Yake, kile alichokita katika mpango Wake. Na halafu basi kama. . .

¹²² Je! uliwahi kuwazia, wakati Kristo alipozaliwa, ya kwamba Mwana wa Mungu, ni kwa nini alizaliwa katika hori, katika banda, na kulazwa horini? Kwa sababu alikuwa ni Mwana-Kondoo. Asingezaliwa nyumbani, wana-kondoo hawazaliwi nyumbani. Na halafu je! uliona hapo walipompeleka Kalvari, na jinsi asingeweza kutoroka. Alikuwa ametwikwa msalaba huu. Alipigwa hata mgongo Wake ulikuwa ukitoka damu. Na, bali walimwongoza, walimwongoza Mwana-Kondoo machinjioni. Unaona? Yeye alikuwa ni Mwana-Kondoo. Vema, na kama shuhuda hizi zote za maumbile, kile alichokuwa... Je! wana-kondoo huzaliwa lini, Desemba ama Aprili? Hakika. Mnaona, ni upuuzi tu, mnaona, kuwazia jambo kama hilo.

¹²³ Hili lilifanywa na kanisa Katoliki la Kirumi kabla halijakuwa kanisa Katoliki huko Roma. Yapata 606 B.K., mahali fulani hapo, ama 306, hasa. Sasa, tunaona ya kwamba makafiri wa Kirumi walimwabudu Jupita, ambaye ni mungu-jua; pia walimwabudu Ashtorethi, ambaye alikuwa mungu-mwezi, ama vinginevyo mama wa...ma—mama wa mbinguni. Vema, kulielezea hili dhahiri, wao walisema ya kwamba Ashtorethi, ama mungu, mama wa mbinguni hakuwako tena, naye alijiakisi katika Mariamu. Kwa hiyo ingali ilibaki ni ibada ya sanamu, ikiunganisha Ukristo na uabudu sanamu.

¹²⁴ Halafu pia, na waliteseka, ama waliabudu na kuiheshimu siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua wao, ambaye alikuwa ni Jupita. Ni wakati ambapo jua kutoka tarehe moja Desemba mpaka tarehe ishirini na tano Desemba, halibadiliki, linapitia kaprikoni yake. Na, jambo lingine, nina kipande kutoka kwenye gazeti ninachotaka kuwasomea siku moja, litawashtua tu. Mnazungumza juu ya yale yaliyotukia hapa chini mtoni siku ile, ninataka kuwaonyesha uvumbuzi huko Yerusalemu kuthibitisha jambo hilo, majuma machache tu yaliyopita, kutoka kwenye gazeti. Kitu fulani walichopata huko Yerusalemu majuma machache tu yaliyopita, kitathibitisha dhahiri kutokea kwa yule Malaika huku chini wakati uo huo na kuituma huduma hii. Naam. Mnaona? Sasa, kamwe sikujua hilo hadi majuma machache tu yaliyopita, nalo hili hapa kwenye gazeti.

¹²⁵ Sasa angalia wakati lilipovuka hiyo, ni ninii—ni katika hiyo, unaona. Sasa, baada ya Desemba ishirini na moja, siku zitaanza kuwa fupi kidogo tu kila moja, ama kuwa ndefu zaidi kila siku, mpaka linashuka chini karibu kwenye Julai. Ndipo inanza kufupika tena mpaka inafikia moja kwa moja...Na huo ni wakati tu wa kuburudika. Nao wapagani wa Kirumi walisema ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua. Tangu tarehe moja Desemba, ama tarehe ishirini na moja Desemba mpaka tarehe ishirini na tano Desemba, walikuwa na sa—sarakasi ya Kirumi, mbio za magari ya farasi na kadhalika ilikuwa ni wakati huo, kwenye wakati huo. Vema, basi, wakati Wakristo ama Wakristo wa Kirumi, wakiongezea mafundisho

yao ya sharti ili kupata pande zote mbili, upagani na Ukristo, walisema, “Kama ni siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua, hebu na tuifanye tu kuwa ni siku ya kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu.” Hiyo hapo siku yako ya tarehe ishirini na tano Desemba kwa ajili ya misa yako, misa ya Kristo. Loo, ni jambo baya jinsi gani! Mnaona?

¹²⁶ Sasa, kuunganisha. Mbona, unasema, “Hivi si siku yoyote ile itafaa?” Naam, bali kumhusisha Kristo na ukafiri? Kitu kile kile alichokuja kukiangamiza, wao wanamhusisha nacho tena. Unaona? Hilo ndilo kosa. Naye Baba Krismasi, mzee fulani huko Ujerumani, jina lake Kriss Kringle, angezunguka-zunguka akiwapa watoto zawadi kwenye siku ya misa ya Kristo, alikuwa ni Mkatoliki nao wakamfanya mtakatifu, sasa ni Mtakatifu Nikolasi. Unaona? Afadhali ninii tu... Wataninii... Hilo, mnajua hilo hata hivyo. Unaona, tunao katika *Nyakati za Kanisa*.

¹²⁷ Lakini asubuhi ya leo, kile ninachotaka kusema ni hiki, ya kwamba, siku hii ijayo ya Krismasi inaukuta ulimwengu ukiwa hauna hali nzuri zaidi ya jinsi ulivyokuwa miaka elfu moja mia tisa ama elfu mbili iliyopita wakati Kristo alipokuja. Si tofauti hata kidogo. Ni karibu hali ile ile uliokuwamo wakati huo, ndivyo ulivyo sasa. Wao... Kama ningefikia uamuzi kutoka kwenye kile... ama somo kutoka kwenye kile ninachotaka kusema, lingekuwa: *Kuporomoka Kwa Ulimwengu*.

¹²⁸ Wakati Kristo alipokuja kwenye Krismasi, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, ulimwengu ulikuwa ukiporomoka, kila kitu kilikuwa kimefikia machafuko. Ulimwengu wa dini ulikuwa umechafuliwa. Ulimwengu wa Kirumi, kimaadili, ulikuwa kwenye kiwango chake cha chini kabisa. Loo, utovu wa uadilifu wa ulimwengu! Wayahudi walikuwa wamemwacha Mungu wao na kuchukua sikukuu yao takatifu iliyoamriwa na walikuwa wameifanya kawaida ya mapokeo. Mungu alikuwa amewaacha. Nao walijua ya kwamba hapana budi jambo fulani litatukia, ulimwengu mzima ulijua, kwa sababu, kuuweka pamoja. Ulikuwa ukiporomoka. Na kitu *fulani* cha kuuweka pamoja, kila taifa katika njia yao wenyewe lilikuwa likitafuta kitu fulani ama mtu fulani aje alishikilie pamoja.

¹²⁹ Kama hiyo siyo picha ya siku hizi, siujui ulimwengu. Unatafuta kitu fulani cha kuushikilia pamoja! Ni kama tu ilivyokuwa miaka elfu mbili iliyopita. Ulimwengu, miaka elfu mbili iliyopita, ulikuwa ukimtarajia Masihi ashikilie kitu hicho pamoja. Lakini miaka elfu mbili iliyopita, Mungu aliupa ulimwengu Masihi. Kwa sababu kama tunatarajia kitu na tunatafuta kitu, Mungu atatutumia. Na sasa ulimwengu, baada ya miaka elfu mbili, umeirudia hali ile ile uliokuwamo miaka elfu mbili iliyopita. Unaporomoka, mataifa, hakuna—hakuna msingi mahali popote. Ukomunisti, Ukatoliki, Uprotestanti, siasa, uadilifu, kila kitu kimesambaratika.

¹³⁰ Nao wanaomba wapate Masihi. Lakini hili hapa ninalotaka kusema! Kama angekuja, je! tungempokea ama tungefanya kama walivyofanya? Je! tungemkataa? Je! tunajua kweli kile tunachohitaji? Wakati mwingine tunataka, tunaomba kwa ajili ya shauku zetu, na wakati mwingine shauku zetu si mahitaji yetu. Hatuna budi kutambua ya kwamba hatuelewi kile tunachohitaji; tunafikiri tunaielewa. Lakini Mungu aliahidi kukidhi mahitaji yetu, na hilo atafanya.

¹³¹ Sasa, vipi kama Joseph wangu mdogo, mwenye umri wa miaka saba, angetaka kwenda kuwinda pamoja nami, naye angelia na kupaza sauti achukue bunduki yangu ya marisau ya kujiendesha, ajaze risasi, “Ninaweza kumwua sungura, Baba”? Vema, ni—nisingemruhusu kufanya jambo hilo, hata hivyo a—anafikiri anaihitaji, bali ninajua zaidi kuhusu hilo kuliko anavyojua. Na vipi kama mtoto wako mchanga mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu angekuona ukijinyoa na wembe mnyofu, na kupaza sauti na kuulilia huo wembe? Hata hivyo amekuona ukijinyoa, anataka kufanya jambo lilo hilo. Mbona, unajua kilicho bora kwake. Hata hivyo u—usingemruhusu auchukue, kwa sababu, kama wewe ni baba mwenye akili timamu usingefanya jambo kama hilo, bali ungeuweka mbali naye. Na kwa hiyo mara nyingi ni kwamba tunataka kitu ambacho ni kinyume cha ujuzi wa Mungu wa kile tunachohitaji, kwa hiyo asingetupatia.

¹³² Nao walikuwa wakiomba wapate Masihi. Walitaka Masihi. Lakini jambo ndilo hili hapa, walimtaka jinsi ambavyo—ambavyo walitaka. Na Mungu akamtuma kwa jinsi Yeye alivyomtaka, nao wakamkataa.

¹³³ Nao wanafanya jambo hilo tena siku hizi, wanafanya jambo lilo hilo leo, wangemkataa tena. Wanafanya jambo lile lile sasa kama walivyofanya wakati huo. Kwa nini? Kwa sababu ile ile, sababu ile ile. Alikuwa wakati huo, nasi tunajua alikuja. Alikuwa, na kwao, bali hakuja katika mtindo na katika njia waliyomtaka aje. Na kama Mungu angetutumia kitu fulani siku hizi, sisi tukikiomba, na kanisa, na wakati Mungu anapokituma hatukitaki. Hakiji kuridhisha ladha yetu ya kimadhehebu. Wakati mwingine hakiji kuridhisha wa—wazo letu la kitheolojia kukihusu. Bali ni ki—kitu kile kile tulichoomba. Ombi lile lile tuliloomba mbele za Mungu, Mungu alitutumia, nasi tunakikataa.

¹³⁴ Tunataka zawadi ya Krismasi kutoka kwa Mungu, bali tunaitaka jinsi tunavyoitaka. Mungu huituma jinsi tunavyoihitaji. Yeye anajua kile taifa, Yeye anajua kile kanisa linachohitaji. Bali tunafikiri tunajua, bali Yeye anajua ni kitu gani hasa.

¹³⁵ Sasa, kama nilivyosema dakika chache zilizopita, tunakuja kwenye Krismasi hii tena, ulimwengu unaporomoka. Hebu na tuyataje tu mambo machache ambayo niliandika chini hapa.

¹³⁶ Hebu angalieni utovu wa uadilifu wa ulimwengu, kamwe haujapata kuwa katika hali ya kushuka hivi, hata. Ni—nina makala hapa ambayo ningetaka tu kusoma aya kadhaa zake. Yanapatikana katika ga—gazeti, Standard Bearer, la Afrika, linasema, “Kifo cha Uadilifu. Uadilifu wa wanawake, ile tabia nzuri ambayo Mungu aliweka katika familia ya kibinadamu kulinda kanuni zake za maadili, inakufa siku hizi, kwa kuwa wanawake wasio na hatia na wasichana wamempigia mungu wa mitindo magoti yao wala hawasiti kufuatilia aibu zilizovuka mpaka wa wastani wa mitindo ya kisasa.” Nina karibu ukurasa mmoja wake hapa. “Jinsi ambavyo sijapata kusikia kitu kama hicho! Na kuvutia kwa jinsia kunachukuliwa kama jambo halali miongoni mwa Wakristo na wasio Wakristo.”

¹³⁷ Kama vile mimi na Ndugu yetu wa thamani Arganbright tulikuwa tukishuka kuja barabarani mapema asubuhi ya leo, tulikuwa tukizungumza juu ya jambo hilo, ni vigumu kumpata msichana mwenye adabu ya kutosha kuona haya. Wamesikia mizaha mingi sana michafu, na kinyaa, na, mbona, usingesema chochote kuwafanya waone haya. Wakati, miaka michache iliyopita, si zaidi ya wakati nilipokuwa mvulana, kitu kidogo kikienda kombo, uso wao ungebadilika rangi, kitu kidogo kikipita, na sketi ya ndani ya msichana mwingine mdogo ingetokeza shuleni, nami nilikuwa nimesimama, nikizungumza, na wakati alipoangalia huko na kuiona sketi ya ndani ya msichana huyu imetokeza, uso wake wa kitoto ungekuwa mwekundu, na akaondoka hapo nilipokuwa, msichana mwenye umri wa miaka kumi na sita. Mbona, ni ninii...hiyo ni tabia iliyotolewa na Mungu ya kulinda uadilifu wetu.

¹³⁸ Basi unaweza kushangaa ni kwa nini ninakemea upuuzi kama huo tunaopata siku hizi, tukijiita Wakristo, na wanawake wakivaa na kutenda, na wanaume wakivuta sigara, na chochote kile, na kufanya yasiyofaa namna hii. Na wahudumu mimbarani, wakipatana, wala hata wasingekuruhusu kuja mimbarani kuhubiri dhidi ya upuuzi kama huo. Nashangaa kama hatufanyi zaidi sana siku hizi kama walivyofanya huko nyuma miaka elfu mbili iliyopita! Kumbukeni, Israeli walipoanza kufanya jambo hilo, Mungu alimwinua Isaya. Wakati huo ulipoisha nao wakaanza tena, Yeye alimwinua Yereima, na kuendelea moja kwa moja. Na Mungu habadilishi njia yake ya kufanya mambo, Yeye ni Mungu wa Milele. Hawezi kubadilika. Wazo Lake la kwanza la kufanya jambo hilo halina budi kubaki vivyo hivyo.

¹³⁹ Kile tunachohitaji siku hizi ni Ujumbe uliotiwa mafuta na Umasihi wa Kristo. Lakini wao wangeupokea? Wanauombea, bali je! wangeupokea? La, bwana, wasingepokea. Wanausulibisha kama walivyofanya mara ya kwanza. Moyo wa mwanadamu ni mdanganyifu.

¹⁴⁰ Uadilifu, ugomvi wa taifa. Ni wapi ulimwengu ulikuwa tayari zaidi kuporomoka katika uadilifu kuliko ulivyo siku hizi?

Na ni nani aliyeweka ninii—ni nani aliyeweka mwendo huo? Sisi Wamarekani. Nilipokuwa hu—huko San Angelo Roma, hapa si muda mrefu uliopita, karibu na yale makaburi ya mapango ya San Angelo, kulikuwako na ilani kule juu kwa wanawake wa Marekani, kwamba “Tafadhali vaeni nguo, mpate kuwaheshimu wafu, kabla ya kuingia kwenye mapango haya.” Taifa la kidini, linalodhaniwa kuwa ni taifa linalomcha Mungu! Tunaishi kwa maadili ya siku zilizopita ya watu wengine, babu zetu ambao walikuwa ni Wakristo.

¹⁴¹ Ugomvi wa taifa. Hapajakuwapo na wakati ulimwenguni ambapo ulimwengu huu ulipokuwa na ku—ku—kuvunjika—vunjika kwa taifa na kuporomoka kuliko ulivyo leo. Mbona, angalieni maoni ya wahariri na matangazo ya habari na—na watoa maoni na wabashiri, na kadhalika, wakisema juu ya mabomu na yale wangeweza kufanya, taifa lolote dogo tu, kuuangamiza ulimwengu wote. Wala hakuna amani miongoni mwao. Huwezi kuleta amani jinsi hiyo. Amani na ushirikiano haviwezi kuja kwa—kwa siasa, huja kwa Kristo. Hawataki kuipokea.

¹⁴² Jinsi ningeweza kuzungumza mambo fulani hapa! Uozo katika siasa zetu wenyewe, mbona, siasa zimeza sana! Mlikuwa mkiisikiliza *Monitor* hivi majuzi usiku, nadhani, ama nafikiri tangazo hili, saa moja ama mbili kutoka hapa Louisville, ambako wanajiunganisha na taifa zima, nao walikuwa wakitoa, wanafanya hivyo mara kwa mara juu ya mambo mbalimbali, nao waliyatoa juu ya Bw. Nixon kuziacha siasa wakati aliposhindwa kura, kura za kisiasa huko Los Angeles, ama kupitia California, na “Je! kamwe angerudi?” Na wakati matangazo hayo, baada ya saa mbili ama tatu, nilikuwa nimeyasikiliza nikishuka kutoka kwenye nyumba ya Ndugu Charlie hapa, na nikayasikiliza nikija huku, mimi na Ndugu Wood, kwenye redio. Na tukaja kukuta kwamba Nixon, kwenye nchi zote za mashariki hapa, mpaka mahali matangazo hayo yalipofika, kutoka Mississippi hadi Pennsylvania, ya kwamba alikuwa amemshinda Bw. Kennedy, na watu wakipiga simu na kutoa maoni, karibu kura nne kwa moja. Ndipo mtu mmoja akasimama na kusema, “Kama msingekuwa—msingelikuwa na mitambo ya kijanja yeye angekuwa Rais.” Haya basi. Siasa, kudanganya, uozo pande zote mbili. Simlaumu, ningejiuzulu, pia, na niache upuuzi huo mbaya uoze, unaangamia pamoja na ulimwengu hata hivyo. Lakini mwinulie Kristo mikono yako na useme, “Mimi huyu hapa naja, Bwana.”

¹⁴³ Mvutano wa taifa. Na sasa ambapo unapaswa kuwazia ya kwamba wanapaswa kuwa wakijaribu kushikana pamoja, wao wametengana sana. Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika ule wakati wa kuja miaka elfu mbili iliyopita wakati ulimwengu ulikuwa ukiporomoka. Unaporomoka siku hizi chini ya mazingira yale yale.

¹⁴⁴ Na halafu upotovu wa kanisa! Loo, jamani! Upotovu wa kidini! Loo, ni upuuzi kuona ulimwengu baada ya miaka elfu mbili ya Biblia na Roho Mtakatifu kuwapo hapa duniani, na siku hizi unaporomoka vibaya sana kama ulivyokuwa miaka elfu mbili iliyopita. Upotovu wa kidini. Siasa ziliingia dini, na dini ikaingia siasa. Ni jambo baya sana kuona hali hiyo! Ninajua ni baya. Mnasema, “Ndugu Branham, hupaswi kuwa ukituchorea picha kama hiyo hapa wakati wa Krismasi.” Mnapaswa kujua kweli, kile mnachopaswa kujua! Sasa, inawezekanaje. . .

¹⁴⁵ Mungu atabariki, bali baraka hiyo inapaswa kuja chini ya hali fulani za mambo, matakwa fulani ambayo huna budi kutimiza. Na iwapo hutatimiza matakwa hayo, basi baraka na ahadi za Mungu hazina kazi kwako. Mungu aliahidi kukutana na Israeli mradi tu waliweka sikukuu zilizoamriwa na kadhalika, kwa—kwa utakatifu na uaminifu. Mungu alikutana nao. Lakini wakati yeye, waliendelea kuifanya kama tu kawaida ya familia, ndipo Mungu akakataa kufanya hivyo tena. Yeye alisema zilinuka usoni Mwake. Kwa hiyo ni jambo lile lile siku hizi, kwamba sisi—sisi—sisi hatuna budi kurudi kwenye ukweli wa jambo hilo.

¹⁴⁶ Mgongano wa kisiasa katika makanisa! Tunasimama siku hizi na karibu madhehebu mia tisa mbalimbali ya Ukristo, kila moja likipiga vita lingine. Vema, hiyo ni, hali haikuwa ni mbaya hivyo wakati Yeye alipokuja, kulikuwako na makundi manne ama matano yao, Mafarisayo na Masadukayo, na kadhalika. Lakini sasa tuna mia tisa na kitu. Mbona, kanisa lipo katika, ni hali mbaya zaidi, kwenye Krismasi hii, kuliko lilivyokuwa kwenye Krismasi ya miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Limekuwa katika hali mbaya zaidi sasa. Mvutano wa kimadhehebu! Kile kilichosababisha hayo yote, rafiki, ni kwa sababu siasa zilipachukua mahali pa Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu anataka kulichukua Neno la Mungu na kuliongoza kanisa kwenye ushindi, lakini utaratibu wa elimu na utaratibu wa siasa, kanuni za imani na madhehebu zimielelekeza kwenye pande mia tisa mbalimbali. Kwa hiyo kanisa halina. . . Kile kinachoitwa “kanisa.” Simaanishi Kanisa halisi; Hilo lingali linaendelea kuwaka moto, loo, naam, Lingali liko vile vile. Lakini kile kinachoitwa “kanisa” ulimwenguni, hicho kinaonekana kuwa ndicho m—mfumo unaoweka ninii. . . unaoushikilia ulimwengu pamoja, ambao unaunganisha kile tunachoita siku hizi uadilifu na mambo ya ulimwengu, limechafuliwa. U—uadilifu wake umeoza, nalo. . . mchwa wa uchoyo, na umekula misingi yenyewe kutoka chini. Hakika ni kweli. Sasa liko kwenye hali Hii ilisema litakuwa, Timotheo wa Pili 3, “Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu,” na kadhalika.

¹⁴⁷ Basi tunapoona siasa katika hali zilizomo katika mataifa, na tunaona makanisa katika upotovu wao katika madhehebu

yao, na hata hivyo tunamtaka Mungu aje kwetu katika mambo hayo. Mungu hatashuka pamoja nasi kwenye mchirizi huo, chini ya mambo tunayomtaka apitie. Hatafanya hivyo. Yeye ni mtakatifu na Yeye—Yeye—Yeye anajua yaliyo bora zaidi. Kama tukiita, Yeye hutujibu. Na wakati anapotuma jibu, tunalikataa. Tunalitaka jinsi tunavyolitaka. Na tunajaribu kumpata Mungu, na kujaribu kujiokoa wenyewe, kwa kitu kile kile kilichothibitishwa kwetu. Enyi Kanisa, nawasihi msikie jambo hili! Jambo lile lile ambalo limethibitishwa kwetu kiungu, ambalo limetuchafua, na hata hivyo tunautazamia mfumo uo huo kutuokoa. Rudini kwenye Neno! Hivyo ndivyo Masihi angesema. Sasa, bali tunaangalia si—siasa. Tunajaribu kwenda kwa ulimwengu wa kitaifa, tunajaribu kuliokoa kwa siasa. Kanisa linataka ulimwengu wetu uokolewe (ulimwengu wa kanisa) kupitia siasa. Jambo hili limeupiga ulimwengu wakati baada ya wakati, tangu wakati wa Musa. Jambo lile lile, siasa zinajaribu kutawala. Na ni potovu. Hakuna jinsi mtu anavyoweza kufanya jambo hilo, kwanza kabisa hakuna kitu kizuri katika mwanadamu. Hiyo ndiyo sababu hana budi kufa.

¹⁴⁸ Na wakati sisi—wakati sisi—wakati sisi tunapouona ulimwengu huu katika hali hii, unaonekana kuporomoka katika kila wakati, ulimwengu unapofikia hali hiyo, watu huomba. Loo, hata Rais anaagiza (kilikuwa ni kitu gani?) dakika kumi ama saa moja ama kitu fulani, za maombi. Hilo halitafaa kitu. Tunachohitaji sio kuomba, bali toba, kugeuka, kuondoka kwenye ninii, kuacha. Mrudieni Mungu! Ni afadhali faraja yangu ijengwe juu ya Neno la Mungu na ubatizo wa Roho Mtakatifu, Uwepo wa Kristo, kuliko usalama wote ambao siasa ama makanisa yangeweza kukupa. Hakika, maana ninajua Hilo litasimama.

¹⁴⁹ Kama hata hatukuwa na taifa tungekuwa ni afadhali, kama tu tungekuwa na taifa la Mungu, Ufalme wa Mungu. Mungu daima hujibu na kuwatumia msaada, bali hawataki kuupokea. Kwamba, Mungu hujibu wakati taifa linapoingia katika hali za namna hii, kila wakati. Wakati ulimwengu, hasa, unapoingia katika hali hii, kuporomoka, basi Mungu daima huwayajibu maombi yao, huwatumia nabii ama kitu fulani, nabii fulani mwenye nguvu kulilipua. Bali hawatamsikiliza. Wanafanya nini? Wanamweka kaburini. Yesu alisema, “Ni nani kati yenu, baba zenu hawakuwaweka manabii huko nje kaburini, kisha wakayapaka chokaa, kuyafanya meupe sasa, na kujenga makaburi yao? Nanyi ndio mliowaweka mle ndani.” Hiyo ni kweli. “Ni nani kati yenu?” Walililia msaada. Mungu akawatumia, nao wakaukataa. Basi nini, je! Mungu Ndiye wa kulaumiwa ama watu ndio wa kulaumiwa? Watu ndio wa kulaumiwa. Hakika.

¹⁵⁰ Wakati Yesu alipozaliwa, ulimwengu huo, kama nilivyosema, unaporomoka. Ulitawaliwa na siasa, na siasa zilikuwa

zimepotoka katika siku hizo. Kanisa la kitaifa lilikuwa limepotoka. Warumi na Wayunani walikuwa wakimtarajia masihi aliyetiwa mafuta. Wayunani na Warumi ambao labda walikuwa na sehemu iliyo nzuri sana duniani, nao walikuwa wakipigana, wao kwa wao, kwa hiyo wao—walikuwa wakimngojea masihi aliyetiwa mafuta aje. Nao Wayahudi, walitaka masihi aje. Nao Warumi walikuwa wakimngojea mwanasiasa mkubwa ambaye angesimama huko Rumi, aiteke Uyunani na kuwaambia jinsi ya kufanya hivyo, na Rumi ingeutawala ulimwengu. Uyunani ilitaka mwanasiasa mashuhuri asimame, mwanasiasa aliyetiwa mafuta, masihi, ambaye angesema, “Tuta—tutawateka hao Warumi na Wayahudi, na hao wengine.” Mnaona, huyo ndiye waliyekuwa wakimngojea.

Kama hiyo si picha ya siku hizi, sijui ni nini. Kweli!

¹⁵¹ Siasa zilitaka masihi aliyetiwa mafuta. Nao Wayahudi walikuwa wakimngojea masihi, nao walitaka yule angekuja si kama waliyekuwa naye, walitaka jemadari ambaye angekuja na kuwafukuza Warumi na Wayunani kutoka katika uso wa dunia kwa ajili yao. Huyo ndiye aina ya masihi waliyemtaka. Walikuwa wakiomba kwa ajili ya masihi kama huyo. Warumi walisema, “Tutumie mmoja. Hebu na tumpigie kura mtu aliyetiwa mafuta, mtu mwenye akili, yeye ni bingwa wa siasa, atajua kabisa mbinu za kuwateka Wayunani na ulimwengu wote.” Ulimwengu wote uliosalia ulikuwa ukisema kwa sauti kuu, “Tutumie mtu ambaye ata—atakuwa—atakuwa ametiwa mafuta sana na kipaji cha akili hata atajua jinsi ya kuuteka ulimwengu wote.”

Sasa, kama hiyo si picha ya ulimwengu huu siku hizi, sijui.

¹⁵² Nalo kanisa, likilia, “Tutumie jemadari ashuke aje, na ambaye atatupa kila mmoja wetu silaha, na anajua jinsi ya kutumia upanga na kutwambia mbinu, nasi tutafagilia mbali Rumi, Myunani, na hao wengine watoke juu ya uso wa nchi.” Hivyo ndivyo wanavyotaka kufanya, kutawala! Hayo ndiyo mamlaka.

¹⁵³ Ni kitu kile kile leo hii tunachopata makanisani. Ninyi Methodist, mnamtarajia masihi. Ni masihi wa aina gani? Si yule ambaye Mungu angewatumia. Ninyi Wabaptisti, mnamtarajia masihi. Ninyi Assemblies of God, mnamtarajia mmoja. Ninyi Wa Umoja, mnamtarajia mmoja. Hiyo ni kweli. Lakini mnatafuta nini? Kitu kile kile ulimwengu wa kisiasa unachotafuta. Mtu fulani mashuhuri mno aliye na kipaji cha hisabati, msomi hodari aliye na D.D., Ph.D., aje kanisani mwenu, ambaye atayabwaga chini madhehebu haya mengine na kuyafanya yote yajiunge na lenu. Jamaa fulani ambaye ni hodari sana katika kushawishi watu kubadili dini hata anaweza kukichukua kitu hicho chote.

¹⁵⁴ Mnaliamba sana kumpata masihi hapa katika wakati wa Krismasi. A-ha. Walipata nini? Wao—walimtaka. Wanataka

kutawala. Ulimwengu siku hizi unataka kutawala. Kanisa linataka kutawala, kila dhehebu. Lakini angalia kile Mungu alichowapa! Walitaka mtu mwenye kipaji cha kijeshi. Walitaka m—mtu mwenye kipaji cha kisayansi, bali Mungu aliwapa Mwana-Kondoo, Mtoto mchanga. Ni tofauti ya jinsi gani! Mnafikiri wangemkubali huyo Mtoto aliyekuwa akilia? Lakini huyo ndiye waliyemhitaji. Mungu hukupa kulingana na haja zako. Hakika. Wao... Alipata... Walimpata Mtoto mchanga wakati walipokuwa wakitaka jemadari; bali walimpata Mtoto mchanga, mpole, mnyenyekevu. Mungu alijua haja zao, hata hivyo.

¹⁵⁵ Yeye kamwe hakuja apate kuwa mwanasiasa wa taifa ama wa kanisa. Na kama Masihi angekuja leo hii, asingekuwa mwanasiasa wa taifa wala wa kanisa. Na kama tukimlilia mtu kama huyo, Mungu atatutumia ukombozi, bali hatuna budi kuupokea jinsi ambavyo anautuma. Hawakufanya hivyo, hawakuutaka jinsi hiyo. Kanisa linaita kwa sauti kuu siku hizi, “Ee Baba wa Mbinguni, waweza kututumia Yesu tafadhali? Utamtuma tafadhali?” Na wakati Roho Mtakatifu anapoanza kuingia ndani, “Loo, hiyo ni... Hatumtaki huyo.” Unaona? Vema, mnakuwa, “Loo, loo, hatumtaki mtu huyu atutawale. Loo, sitaki kusikia Hilo. La. Jamani... Nisingekubali Hilo, dhehebu langu halitaamini Hilo.” Basi humtaki Masihi, hutaki upako. Kama Mungu angemtuma Masihi, angekuwa hasa Neno kwa Neno la Biblia, vile vile hasa alivyokuwa mara ya kwanza. Kilio cha ulimwengu, wakati tunapowaona wanasiasa na kila kitu wakiubana sana na kuutoa Uhai wenyewe wa kanisa, nasi tunalia, na Mungu akatutumia, kisha tungeukataa. “Hiyo ni kweli, tusingeutaka. La, kama haukuendana na i—imani yetu ya kimadhehebu, tusingeupokea.” Mnaona? Loo, hivi hamwoni kile Krismasi halisi... Watu hawautaki. Hawataki njia ya Mungu ya kuutuma. Wanatafuta kitu fulani, bali hawautaki.

¹⁵⁶ Sasa, Mungu aliwatumia, katika siku waliyokuwa wakililia, si mtu mwenye kipaji cha kijeshi, si jemadari mkuu akishuka akija na bakoli na bamba la chuma, na upanga wa miujiza ama mkuki ambao angeweza kuwarushia na kuwafukuzia Warumi na Wayunani na hao wengine baharini na kuwazamisha tena. Yeye hakuwatumia kitu kama hicho, ingawa alisema kweli alifanya hivyo wakati mmoja katika Musa, lakini walilihitaji wakati huo. Lakini aliwatumia Mwokozi wala hawakumtaka. Walidhani kulikuwa na... waliokolewa. Mnaona? Hivyo ndivyo ilivyo na makanisa siku hizi. Yanapatikana kwenye Krismasi hii na mapambo yote ya kumetameta ya Krismasi, taa za Baba Krismasi, sifa za kipagani na kadhalika zilizotumbukizwa ndani ya makanisa ya Katoliki na ya Protestanti, na yamepotoka yawezavyo kuwa. Na Mungu anawatumia Mwokozi. Ni kitu gani? Kurudi kwenye Neno. Roho Mtakatifu, Masihi wa Mungu, Mtiwa Mafuta Wake, kulitia kanisa Lake mafuta na kulirudisha

kwenye Neno. Unafikiri wanalitaka? La, bwana. Hawatalitaka. Watalikataa kama wanavyofanya sikuzote.

¹⁵⁷ Yeye hutuma Mwokozi, lakini anawatumia Mwokozi kwa sababu gani basi? Ninataka kuingiza kitu fulani kidogo hapa kitakachowasaidia. Kuna watu waliochaguliwa tangu zamani watakaolipokea. Walikuwako wakati Yeye alipokuja kwa mara ya kwanza, watakuwako wakati atakapokuja kwa mara ya pili. Haidhuru ulimwengu wa kanisa unawazia nini juu yake, baadhi... Yeye hamtumi bure. Mtu fulani atampokea. Kuna mtu fulani atakayelipata, hivyo tu; bali si ulimwengu wa kisiasa wala kanisa la kisiasa, ama chochote kile. Lakini wakati unapolia Naye Mungu anamtuma, mtu fulani ata—atampokea. Hiyo ni kweli.

¹⁵⁸ Yeye alimtuma Mwokozi, sio kuyakanyaga-kanyaga mataifa. Kama vile tungewazia siku hizi, tunahitaji mtu anayeweza kusimama imara. Marekani inataka mtu atakayeibomoa Urusi isiwepo kabisa. Urusi inataka mtu atakayeuangamiza ulimwengu wote na kuwapeleka mwezini. Lakini Mungu hutuletea amani. Mungu hutuletea tumaini. Hatuitaki. Loo, mwasema, “Tu—tunaweza kuwa na amani, mataifa yanataka amani.” Hakika. Nao wanafikiri wanaweza kuipata wakati U.M. utakapokutana. Vema, U.M. uko mbali sana vile vile kutoka kwake. Amani ya ulimwengu huu, uliyo nayo siku hizi, ni kama puto la mpira linaloelea hewani, upepo wowote mdogo tu unaweza kuipeleka upande wowote unaotaka. Hakika. Badiliko lolote dogo la siasa linaliyumbisha kutoka upande mmoja hadi mwingine. Mtu huwezi kufanya maombi katika U.M. kwa maana huenda yakadhuru jina la watu wengine, hisia ambazo hata haziamini Mungu. Huo si uthabiti, unalipulizia tu upande wowote? Na jambo lingine, puto litapasuliwa na chochote, pia. Amina. Na hii inayoitwa amani ya ulimwengu, na U.M. na kadhalika, italipuka. Kweli. Hakuna amani katika hilo. Mtu huwezi kupata amani kwa mafanikio ya kujibunia ya mwanadamu. Haipo. Inachukuliwa na kila upepo!

¹⁵⁹ Kanisa linaitaka. Wanataka...amani yao ni kama... hupeperushwa na kila upepo wa fundisho, pia. Kila kitu kinapitia hapo, mmoja wao anasema, “Loo, nafikiri yote yanayotupasa kufanya...”

¹⁶⁰ Ati unafikiri? Huna kufikiri kokote kunakokuja. Mungu tayari ameelezea mawazo Yake. Huna haki ya kuwazia. “Nia iliyokuwa ndani ya Kristo na iwe ndani yenu.” Naye alikusudia na akafanya mapenzi ya Mungu. Yeye alisema, “Kama sizifanyi kazi za Mungu, basi msiniamini Mimi.” Unaona? Huna kufikiri kokote kunakokuja. Yeye ndiye anayewaza. Hebu nia Yake iwe ndani yako, utawazia tu vile vile, na hilo ni Neno Lake. Utawaziaje vinginevyo? Yeye tayari ametoa mawazo Yake kwetu. Lakini tunataka kuwazia sisi wenyewe, “Nafikiri wanapaswa kufanya hivi.”

¹⁶¹ Nilikuwa nikiendesha gari na mpendwa mzee fulani jana, tukipanda kwenda kumwombea mtoto mgonjwa. Na tulipomfikia mtoto huyo mgonjwa, familia hiyo haikutaka tumwombee, lilikuwa tu ni wazo la mtu huyu. Hata hivyo, tulipokuwa tukienda barabarani, mama huyu alisema, mama mzee mwenye umri wa karibu miaka themanini na moja, mwanamke mwerevu, mwenye akili nyingi, mzuri sana, lakini akasema, “Nafikiri kile kinachopaswa kutukia,” (mnaona, “nafikiri”) “ni kwamba makanisa yote yanapaswa kuungana pamoja na kuwa moja.” Hivyo ndivyo ibilisi anavyowazia hasa. Lakini Mungu anataka utengano wa kanisa Lake na mambo ya ulimwengu. Yeye hataki lichanganyikane na siasa za kanisa. Unaona? Na vipi kama Mungu angemtuma Masihi ulimwenguni? Na hilo ni... Mama huyo alikuwa akiwazia tu mawazo ya ulimwengu mzima. Muungano wa Makanisa ni nini ila wazo lile lile? Baraza la Makanisa Ulimwenguni ni kitu gani ila kusudi lile lile kufanikisha wazo lilo hilo? Hiyo ni kweli? Vema, basi, mama, mama huyo alinena tu mawazo ya ulimwengu.

¹⁶² Lakini haya hapa mawazo ya Mungu katika Biblia. Hatuna haki ya kuchukua tofauti na Hayo. Hayo ni mawazo ya Mungu yaliyoelezewa kwetu. Tunaona, tunauona ulimwengu ukiporomoka, nasi tunalilia jambo fulani. Hebu na tulipokee. Sasa, kama likipokea na kujaribu kutuelekeza kwenye siasa, hicho ndicho kitu hasa kilichotupotosha.

¹⁶³ Nina jambo dogo la kumwambia kiongozi wa kitaifa wa hili Wafanya Biashara Wakristo. Ni kundi zuri la watu, lakini wakianza kuelekea kwenye njia mbaya, watageuka kuwa poda kama hao wengine, watakuwa dhehebu. Na ninawatakeni mniombee na mumwombee mtu huyu. Sina budi kwenda, nina ono kutoka kwa Bwana kwa ajili yake. Mnaona? Na kama hawatafanya mabadiliko hayo, kama wakiendelea, watafanyika dhehebu. Na, wakifanya hivyo, Mungu amemalizana nao. Hiyo ni kweli.

¹⁶⁴ Mnaona, watu hawawezi kuungana pasipo kujaribu kupata mawazo yao wenyewe. Hiyo ndiyo sababu Mungu huwachukua watu binafsi. Mnaona? Mungu hashughuliki na kamwe hajapata kushughulika na dhehebu. Hakuna mahali katika historia alipopata kufanya hivyo. Yeye huwashughulikia watu binafsi, mtu mmoja. Hiyo ni kweli. Lakini tunajaribu kukusanya kundi la watu pamoja na kusema “ni *hivi* na *vile*,” na kadhalika. Muda si muda mwajua, watu mashuhuri, werevu, wenye akili nyingi, majitu haya ambayo ibilisi ameyatuma humo, yanaingia na kusema, “Vema, inapaswa kuwa *hivi*. Ninaweza kuwathibitishia.” Haidhuru unaweza kuthibitisha nini, kama ni kinyume na Neno hilo, kaa mbali nalo. Hiyo ni kweli. Wamechukuliwa na kila upepo wa fundisho. Unalipulizia popote na linalipuka wakati wowote. Ni kweli.

¹⁶⁵ Urusi siku hizi inamtafuta masihi aliyetiwa mafuta. Wanatafuta nini? Vipi kama Mungu aliwatumia Masihi aliyetiwa mafuta, Mwana-Kondoo kama alivyofanya miaka elfu moja mia tisa iliyopita? Wangemwondolea mbali kama tu vile Herode alivyofanya, wangejaribu wawezavyo kumwondosha. Maoni ya Urusi kuhusu masihi ni yapi? Wanataka sayansi. Wanataka sayansi iliyotiwa mafuta, mwanasayansi, mwenye kipaji anayeweza kuushinda ulimwengu kwa ajili yao, anayeweza kuwashinda, walimwengu wengine kufika mwezini, ambaye anaweza kuteka anga za juu sana, ambaye anaweza kuwapeleka mbali kupita nyota. Huyu ndiye aina ya masihi Urusi inamtafuta.

¹⁶⁶ Ee Mungu! Sasa sikilizeni, tuko kwenye wakati wa Krismasi tena. Vipi kama walimpata? Basi tarajieni kitu tofauti na hilo. Ingekuwaje kwa hao watu wengine ambao Mungu aliwaumba? Mnaona? Mnaona, Mungu anajua tunachohitaji, si tunachotaka. Sasa jifunzeni hilo. Vipi kama Urusi wangempata mpakwa mafuta wao? Sasa, wasingempokea Mwana-Kondoo. La, la, wasingempokea yeyote. La, bwana, hawamtaki. Ni hayo tu, hawamtaki tu kabisa. Hawataki kitu kama hicho. Wanataka masihi aliyetiwa mafuta. Vema, *masihi* maana yake ni “aliyetiwa mafuta.” Kwa hiyo basi kama wanataka aliyetiwa mafuta, ila wanataka mwanasayansi aliyetiwa mafuta, mwenye kipaji anayeweza kuchukua atomi na kuzipasua, anayeweza kuteka anga, ambaye angeweza kuihamishia Urusi mwezini na kuangalia nyuma na kujipigapiga kifuni, na kusema, “Ninyi walimwengu wengine ni mbwa, tutumikieni.” Jambo ndilo hilo, hilo ndilo Urusi inalotaka. Loo, naam, bwana. Mwajua, ulimwengu mzima unalilia. . .

¹⁶⁷ Ujerumani ililia ipate mmoja wao si muda mrefu uliopita. Wakampata mmoja. Angalia walichopata naye, pia. Mnaona? Mnaelewa, sivyo? Walimpata Hitler. Nao walijiingiza kwenye kitu gani? Machafuko. Hicho ndicho hawa masihi waliopakwa mafuta wanachoishia kama mkimkataa Masihi wa Mungu. Walipata kitu gani? Wakati baraka za kipentekoste zilipoishukia Urusi, ama Ujerumani, waliukataa Ujumbe huo. Waliwacheka na kuwaweka gerezani. Walifanya nini? Waliukataa Msalaba, nao wakapata usaliti, ile swasitika. Usipoipokea rehema, basi hakuna kilichosalia ila hukumu. Hiyo ni kweli, rafiki. Sasa angalia mahali walipo siku hizi. Unaona? Angalieni, hawana uwanachama popote, wao ni watu waliovunjikavunjika. Walimkubali masihi wa uongo. Na kama Urusi ingempata mmoja kama huyo, haidhuru wangekikubali kipaji chao jinsi gani, itakuwa ni vile vile. Italiangamiza taifa zima. Mnaona?

¹⁶⁸ India siku hizi inataka mtiwa mafuta. Wanamtaka masihi. Sasa kumbukeni, *masihi* maana yake ni “aliyetiwa mafuta.” Wanataka mtiwa mafuta. Wanataka nini? Wanamtaka mmoja atakayewalisha, awape chakula; awavalishe, bila ya kuyafanyia

kazi, watembee tu huku na huko mitaani na kukirusha kutoka upande mmoja hadi mwingine. Haya basi. Hawatafanya kazi, wanataka tu kuombaomba. Kwa hiyo wanataka namna fulani ya mtu mtakatifu ainuke ambaye anaweza kufikia vilele vya miti na kuvitikisa, mkate na nyama na—na kadhalika, vianguke, juu yao, na wao waketi kitako hapo na wale, na kulala siku nzima, kisha waamke na wavae nguo zilizo bora sana, na huyo—huyo ndiye aina ya masihi ambaye India inataka.

¹⁶⁹ Urusi inataka mwanasayansi mwenye kipaji awe masihi wao aliyepakwa mafuta Krismasi hii. Huyo ndiye wanayetaka wapewe. India inataka masihi ambaye anaweza kuwalisha na kuwalisha nguo, bila kufanya kazi.

¹⁷⁰ Marekani, je! mnataka nini? Maoni yenu ni yapi, enyi Marekani? Mmekuwa mkilia mpate masihi. Ninajua ya kwamba haya yanarekodiwa. Mmekuwa mkilia mpate masihi. Mnataka nini? Mmepata mlichotaka. Mlitaka mwanasiasa, nanyi mmempata. Sasa mtafanyaje na jambo hilo? Atawachuna ngozi, hivyo ndivyo atakavyofanya hasa, atawapeleka kaburini mwenu. Mlitaka jambo hilo, mmepata shauku yenu. Sasa mtafanyaje na jambo hilo? Liko mikononi mwenu sasa, Ahabu na Yezebeli mamboleo. Kitu kile kile mlichokitoroka mkaja hapa mpate uhuru, mlifikokota moja kwa moja mkarudi kwacho tena, lakini hicho ndicho mlichotaka. Mlitaka Riki anayekata nywele zake kibapa, Elvis mamboleo, mmempata. Mlitaka mwanasiasa msomi na mwerevu, mwenye kipaji cha akili, mnaye. Mlifanyaje jambo hilo? Kwa ujanja, mitambo ya kisiasa kumwingiza, mkawahadaa watu walio wazuri. Sasa, mimi si mwanachama wa Democrat wala mwanachama wa Republican, mimi ni Mkristo. Mnaona? Mnaona? Pande zote mbili zimeoza. Lakini wakati mtu ambaye angalau alionyesha mawazo na matumaini ya Ukristo upande huo mwingine, na halafu mnageuka na kutega mitambo (ya kufanya nini?) ya kumchagua mtu mwenye kipaji mliyemtaka. Mlifanyaje jambo hilo? Mlimweka kwenye televisheni, mkairusha kote nchini, loo, jamani, mkijaribu kupima nguvu za bongo kati ya hao marais wawili wateule. Kuwa ninii... Mlimchagua yule mliyedhani ana bongo lenye kipaji, bila ya kuangalia kilichokuwa nyuma yake.

¹⁷¹ Mnaona mlichopata katika maafikiano yenu? A-ha. A-ha. Loo, ni Krismasi tena. Naam, Marekani ina masihi wake, mtafanyaje naye? Mwangalieni analowafanyia. Hebu kumbukeni tu, kama tu vile Hitler alivyoifanyia Ujerumani. Hebu kumbukeni tu, wekeni hilo mawazoni mwenu. Limerekodiwa. Naam. Mnalo. Hata hivyo, kulikuwa kungali na wa kutosha kutoka kwenye miamsho hii iliyopitia nchini, watu wastahivu wa kutosha waliosalia wenye nia za kumcha Mungu, ambao wanalifanya jambo hilo na kulishikilia kidogo zaidi. Bali mlajibunia wenyewe, kwa mafundi wenu wa mitambo, mtambo

ambao ungeweza kudanganya kwa kura, nayo magazeti yenu yakalitangaza kote nchini, wala hamkufanya kitu juu yake ili kulirekebisha. Lakini mlimpata. Huyu ndiye aina ya masihi waliyemtaka, kwa hiyo nadhani wanaweza wakastarehe, wamempata mtu mwenye kipaji, mwenye akili, hakika, mwerevu, aliyeelimika vilivyo.

¹⁷² Nanyi mnajua vizuri na vema ma—mafundisho ya Bwana wenu, ya kwamba watu waovu wa siku hizi, na wa kila siku, sikuzote wamekuwa ndio watu werevu. Hivi hamjui ilikuwa ni watu wa Kaini ndio waliibuka wanasayansi na wenye kipaji, ambapo watu wa Mungu walikuwa ni wachungaji na kadhalika, moja kwa moja hata kufikia yale maangamizi? Na ilikuwa ni hao wakulima wadogo wanyenyekevu na kadhalika ndio waliookolewa kwenye ile safina, na wenye vipaji wakaangamizwa. Hivi hamjui Yesu alisema, “Wana wa siku hizi, ulimwengu huu, ni—ni—ni werevu kuliko wana wa Ufalme?” Mbona? Wao ni wana-kondoo, wanahitaji kiongozi. Nao wanajaribu kumchagua kiongozi wao kwa elimu, wenye akili hufanya hivyo; bali walio wanyenyekevu humchagua kiongozi wao, ambaye ni Roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo hasa kanisa limefanya, yale majitu ya kimadhehebu ambayo kanisa liliyachagua; wakati, Mwili wa Kristo halisi ulimchagua Roho Mtakatifu na Neno Lake. Inategemea ni kitu gani unachokiruhusu kikuongoze. Mwana-kondoo hana budi kuongozwa, na hapo ndipo tumefikia.

¹⁷³ Sasa wana masihi wao, mwalimu wao aliyepakwa mafuta, mwerevu, mwenye akili sana. Loo, jamani! Kamwe hapajatokea rais aliyesimama aliye mwerevu kama mtu huyo. Mbona, atasimama moja kwa moja na kuweka... Ataninii, nafikiri leo ama usiku wa leo, ama wakati fulani katika siku moja ama mbili zijazo, nilisikia hilo katika matangazo yaliyotolewa hivi majuzi, ya kwamba, mwulize tu swali lolote utakalo. Hakika, ni—ni mtambo tu ulioelimika, huyo ndiye Marekani waliyemtumainia, sasa hebu na tuone mahali mtakapofikia naye. A-ha.

¹⁷⁴ Mliukataa, Marekani, mliukataa Ujumbe wa Kristo, mlimkataa Roho Mtakatifu ambaye alithibitishwa mbele zenu, hata kufikia kwenye makao yenu makuu, ambako nguvu za Kristo zilijidhihirisha zenyewe, zilizoyajua mawazo ya mwanadamu, Yeye angeweza kuwaponya wagonjwa na angeweza kugundua mahali pa siri pa moyo, na kufanya vile vile hasa Mungu alivyosema ingetukia katika siku za mwisho, nanyi mnaukataa. Haukuwa umepigwa msasa vya kutosha. Ulizaliwa katika hori. Ulinuka, kwa taifa. Na, hebu kumbukeni, siasa zenu na ukanisa wenu unanuka mbele za Mungu, pia. Mungu hupenda harufu inayonukia vizuri ya unyenyekevu. Kanisa haliitaki hiyo, unyenyekevu wa uongo. Mungu anataka unyenyekevu halisi. Huo ndio anaoupenda. Sasa wana jitu lao lenye elimu.

¹⁷⁵ Kanisa, linataka masihi. Vema, linataka nini? Linataka aliye na kipaji, mfumo wa kimadhehebu, uliopakwa mafuta ku—kuwafanya wafikie mahali penyewe. Hebu nichukue wakati wangu hapa, ili kwamba mtakuwa na hakika ya kwamba imeeleweka hapa na kila mahali. Kanisa siku hizi linataka mpakwa mafuta mwenye kipaji ambaye amepanga kila kitu barabara kabisa hata wanaweza kuishi ulimwenguni, wanawake wanaweza kukata nywele zao, kupaka rangi nyuso zao, wanaume wanaweza kuoa mara nne ama tano na wangali wawe ni mashemasi, loo, wanaweza kufanya chochote wanachotaka kufanya na wangali watashikilia maungamo yao kwamba ni “Mkristo.” Mtampata!

¹⁷⁶ Hamumtaki Masihi wa Mungu, Neno lililotiwa mafuta, Neno lililodhihirishwa, Neno likijileta mbele. Hamlitaki hilo. Mungu aliwatumia Hilo. Lakini kanisa halimtaki Huyo. Linataka kanuni zao za imani nao wanataka mtu mwenye kipaji anayeweza kuziweka kanuni za imani kufikia mahali ambapo kila kitu kinazisujudu. Mtampata, a-ha, yuko njiani. Mna watoto wengi sana kwake, lakini kutakuwako na babu atakayeinuka moja ya siku hizi, Farao asiyemjua Yusufu. Na huyo ndiye mliyemtaka, huyo ndiye kanisa. . . Mnaweza kuona jinsi wanavyofanya hasa, naam, bwana, jinsi hasa.

¹⁷⁷ Ufunuo 17 inalielezea dhahiri jambo hilo, juu ya yule kahaba wa kale na binti zake. Kweli kabisa. Na wote watarudi nyumbani kwa mama, na wako njiani sasa hivi kuunda kanisa moja la ulimwenguni kote. Mtapata kile hasa, enyi madhehebu, mnachotaka. Nisikieni! Litatimia wakati huo! Na huenda nitakuwa nimeondoka ifikapo wakati huo. Bali wale ambao hawatakubali hilo wakati Nuru za jioni zitakapoanza kushuka na watoke, wataangalia huku na huko, waone kwamba wanalazimishwa kuingia katika kitu fulani na dhehebu lao, nalo dhehebu lao limeichukua wapate kujiepusha na aibu. Jambo ambalo, wote watalifanya. Lakini hao watu wasiotaka mfumo huo, ambao wameukubali mfumo wa Mungu, Roho Mtakatifu na Neno, wanasema, “Hapana budi mtu yule alisema kweli.” Huenda ikawa mambo yamechelewa sana wakati huo.

¹⁷⁸ Tunawaona Waepiskopali, Wapresbiteri, Wabaptisti, kila kitu kikiingia kwenye Wafanya Biashara wa Full Gospel, kila kitu kikijaribu kumtafuta Roho Mtakatifu. Hivi watu hawatambui ya kwamba hiyo ndiyo saa yenyewe ambayo Bwana-arusi alikuja, hapo wanawali waliolala walipojaribu kuja na kununua mafuta? Hapo ndipo Yesu aliposema Bwana-arusi alikuja na kuingia, nao hawakuingia. Watu hawa wana shida gani? Wanapayuka-payuka juu ya jambo hilo, wakati Biblia inathibitisha ya kwamba hawakuingia? Na walipokuwa wakijaribu kufanya hivi, Bwana-arusi alikuja, nao wakatupwa kwenye giza la nje. Ilikuwa ni kitu gani? Huenda walipata kila namna ya mihemuko, kila namna ya mambo ya kujibunia, kila

namna ya—ya mihemuko ambayo huenda ilionekana kama ni thibitisho lake, bali Kanisa tayari limetiwa muhuri ndani na lilikuwa limeondoka. A-ha. Huenda ikawa huo ni unabii.

¹⁷⁹ Wanataka kitu fulani, wanataka kitu fulani jinsi wanaweza kuishi namna yoyote wanayotaka. Wao, hilo ndilo ulimwengu wa kanisa unalotafuta. Mtu fulani ambaye—ambaye wanaweza kwenda kwenye kanisa lililo kubwa kabisa mjini ambako watu wote mashuhuri wanashiriki. Wanaweza kuwa na mnara-pia ulio mrefu zaidi kwenye jengo hilo. Wanaweza kuwa na kinanda kilicho kizuri kabisa. Wanaweza kuwa na vi—viti virefu vya kanisa. Wanaweza kuwa na mhudumu ambaye hatawaambia neno juu ya jinsi wanavyoishi, kama wakitaka kucheza dansi, wanataka kuandaa namna fulani ya maonyesho, wanataka kuvaa kaptura, wanataka kukata nywele zao, ama wanataka kufanya mambo haya, wanaweza kuvuta sigara, ama kunywa pombe kuchangamka. Hayo ndiyo mazoea kanisani. Unywaji pombe wa kisasa tu, kuwafundisha tu watoto wenu kunywa pombe, bali si nyingi mno, wasipitilize mpaka nayo. Kuvuta sigara, bali si—si kupita kiasi. Kuvaa chochote unachotaka, ila u—ujaribu tu kujiweka mstahifu vizuri ujuavyo ama uwezavyo. Unaona? Loo, huo unafiki! Huyu ibilisi aliyetiwa mafuta! Hicho kitu kinachoitwa dhehebu! Kitu hicho kinachoitwa dini! Ni cha ibilisi. Mrudieni Kristo na Neno Lake! Jiokoeni na kizazi hiki kiovu. Tubuni, kila mmoja wenu, kabla ya kuchelewa sana kutubu, na ingeweza kuwa hivyo wakati wowote.

¹⁸⁰ Tunapomwona yule mwanamwali aliyelala akifanya anavyofanya, inaonekana kana kwamba inapaswa kuwashtua watu kutoka kwenye akili zao. Lakini badala ya hilo, wao, “Loo, utukufu, hii si ni ajabu! Haleluya!” Loo, jamani! Hivi watu wanaweza kufika umbali kiasi gani? A-ha. Wanaweza kuingia katika hali ya jinsi gani wakiwa na nia zao za kisiasa, na dhana zao za kisasa, wakiwa hawajui zaidi juu ya Neno la Mungu kuliko mhotentoti anavyojua hekaya za Kimisri. Kweli! Ni dha—dhana tu ya kitheolojia kulihusu, ama kitu fulani cha kisaikolojia ambacho wameingiziwa kwa njia ya kanuni ya imani ama kitu cha namna fulani, na Pentekoste wamejawa sana na hayo. Samahani kwa tamshi hilo. Mambo mengi haya ya wahubiri wanawake na kadhalika, ndiyo mashina ya hayo. Kweli! Na haya basi. Dansi, roki, elimu, hilo ndilo aina ya kanisa a—ambalo ulimwengu unataka. Huyu ndiye aina ya Masihi wanayemtaka, mtu anayeweza kuwaunganisha pamoja. Mtampata. A-ha. Roho yake tayari inatenda kazi miongoni mwa watoto wa binadamu. Hiyo ni kweli. Wangali wanakiri Ukristo, watampata.

¹⁸¹ Mungu aliwatumia, alituma juu ya nanii...sisi katika mwaka wa 1963, kama Mungu angetuma juu yetu katika mwaka wa 1963, upako ule ule alioutuma huko nyuma mwanzoni, tungeukataa kama walivyofanya wakati huo. Kwa sababu, kama

huyo mtiwa mafuta, masihi, alikuja kwa kanisa, angekuwa ni yeye yule kama Biblia ilivyosema alikuwa. Waebrania 13:8, ilisema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Basi kama tukiomba tupate masihi, mtiwa mafuta, ni kitu gani, je! tunataka mwanasiasa wa kidini? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Je! tunataka mtu mwenye kipaji cha kijeshi? [“La.”] Je! tunataka mwanasayansi mwenye elimu? [“La.”] Nanyi mnataka Mwana-Kondoo. [“Amina.”] Mnataka Mwana-Kondoo atakayewarudisha, pasipo wao kujitukuza, bali kurudi kwenye Neno. Kurudi! Yule atakayewaambia Kweli haidhuru ni nini, unaona, dumuni moja kwa moja nalo, aliweke sawa. Hawamtaki. Kama angekuja siku hizi angekuwa kama alivyokuwa wakati huo, angedumu moja kwa moja na Neno la Baba. Angehakikisha ya kwamba kila Neno ambalo lilikuwa limeahidiwa katika Biblia lilidhihirishwa kwa wana wa binadamu. Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁸² Yesu alisema, “Ni nani anayeweza kunithibitishia kwamba Mimi nina dhambi? Ni nani anayeweza kunihukumu kwamba nina dhambi, kutokuamini? Kama kila kitu Baba hakusema ya kwamba ningefanya, kama sijakifanya basi niambieni ambapo nimekosea.” Amina. “Niambieni ambapo sikitimizi.” Amina. Mnajua, dhambi ni kutokuamini. Hiyo ni kweli. Tunajua jambo hilo. “Ni nani anayeweza kunionyesha ambapo sijatimiza,” Yeye alisema, “kila Neno Baba alilosema ningefanya? Ni nani wanaoweza kuninyooshea vidole vyao juu Yangu na kusema sikutenda? Ni nani kati yenu?” Basi kwa nini hawakuacha kumsumbua? Kwa sababu ilikuwa imetabiriwa ya kwamba wangepanya hivyo. Bali Yeye angetimiza Neno la Baba juu ya alama kabisa kama alivyofanya mara ya kwanza. Angelitimiza hilo kikamilifu, kwa maana asingeweza kubadilika, kwa sababu Mungu ni Neno. Kwa maana hilo ndilo alilo hasa, Yeye ni Neno. Naye ni Neno gani? Yeye ni Roho Mtakatifu anayelichukua Neno la Mungu na akalidhihirisha. Hilo ndilo Yesu Kristo hasa... Wakati Mungu Roho, Baba, alipofanyika mwili miongoni mwetu katika umbo la Mwanawe, Yeye alilichukua Neno la Mungu na akalidhihirisha, akalionyesha kwa watu, nao hawakutaka la jinsi hiyo. Walikuwa na kanuni zao za imani, walikuwa na madhehebu yao wenyewe, na hilo lilikuwa ni kinyume na dhehebu lao, kwa hivyo hawakulipokea.

¹⁸³ Na lingekuwa ni jambo lile lile siku hizi. Kama Masihi angekuja, Yeye angeyachukua mambo ambayo Mungu ameyaahidi hapa, na mambo haya katika Biblia, naye angeyadhihirisha mbele ya wana wa wanadamu, na kila dhehebu lingemkataa. Hawamtaki. Hawataki uhusiano wowote Naye. Bali huyo—huyo ndiye Mungu angewatumia. Kama aliwatumia kitu chochote, kingekuwa ni huyo. Na halafu wangemkataa na kujiletea laana juu ya nafsi zao, juu ya jamii hii ya watu, kama tu vile Wayahudi walivyofanya katika siku ile, na hao wengine.

Naam, bwana. Unajua kile angefanya kama Masihi angekuja mwaka wa 1963, unajua kile angefanya? Angevunjilia mbali kila dhehebu tulilo nalo. Angekiweka uchi kitu hicho chote kabisa.

¹⁸⁴ Vema, wao wangesema, “Angemsukuma nani, Daktari *Fulani* ama Daktari *Fulani*?”

¹⁸⁵ Angesema, “Ninyi ni wa baba yenu ibilisi, na kazi zake mnazifanya.” Ndicho hasa kile angesema. Asingecheza nao kwa njia yoyote. Hakucheza nao hapo mwanzo, Naye ni yeye yule leo kama alivyokuwa wakati huo. Chochote kilichokuwa ni kinyume na Neno, angekiita hivyo. Angesema, “Ninyi ni wa baba yenu ibilisi, na kazi zake mnazifanya. Kufanya mambo kinyume na Neno Lake.” Hiyo ni kweli. Na ishara ya Masihi ingemfuata. Hiyo ni kweli. Kumfanya awakabili na kusema, “Hivi Mimi sijatimiza yale yaliyotukia? Ni nani kati yenu anayeweza kunihukumu kwa kutokuamini?” Unaona?

¹⁸⁶ Lakini wangejaribu kumfanya karagosi, wamchukue mahali mahali kama alivyofanya yule Farisayo. Alimshusha kule chini akawafanyie burudani fulani, akaribishe wageni wengi kwake, wakathibitishe kwamba Yeye hakuwa ni Nabii. Mnaajua ile hadithi ninayofundisha juu ya jambo hilo. Mnaona, wangepanya jambo lile lile siku hizi kwa wale angeweza kuwakusanya pamoja awalete apate kuwaburudisha, wangepanya jambo lile lile. Naye angeenda. Haleluya! Angeenda, kwa maana Yeye daima huenda mahali anapoalikwa. Huku akijua yale Farisayo huyo atakayofanya. Alijua ya kwamba Farisayo huyo hakuwa na haja Naye. Alijua kuna mtego amewekewa kwa kisiri mahali fulani. Hao Mafarisayo hawakuwa na shughuli Naye, walimchukia. Na maskini Simoni huyu alimtaka ashuke aje pale ili kwamba aweze kuvutia umati nyumbani mwake. Lakini Yeye alijua hilo. Aliingia moja kwa moja. Je! alimjali? Watu mashuhuri ndio aliowajali. Yeye aliketi huko nyuma na miguu michafu. Lingekuwa ni jambo lile lile siku hizi. Hawamtaki Kristo. Hawaitaki njia ya Mungu, mnaona.

¹⁸⁷ Naam, Yesu angesema, “Ninyi ni wa baba yenu ibilisi.” Na hao watu walishika hiyo torati na kadhalika na kila kitu katika dhehebu lao na kanuni za imani, kikamilifu kabisa, wataosha vyungu. Na Yesu alisema, “Mmechukua kanuni zenu za imani na mkalitangua Neno la Mungu, kwa mapokeo yenu.” Na Waebrania 9:12 inasema pale, ninaamini, la, ni Waebrania 12...la, 9:12, ninaamini ndiyo, mahali fulani hapo, yeye alisema ya kwamba “Tunaposafishwa na kusamehewa, tunasafishwa kutokana na matendo mafu ya kimwili.” Na wakati tunaposamehewa kweli dhambi zetu na Damu ya Yesu Kristo, Roho Mtakatifu anaingia ndani yetu nasi tumekufa kwa matendo ya kimwili. Loo, enyi kanisa la Kipentekoste, kwa nini mlifanya kosa kama hilo? Enyi vipofu mkiwaongoza vipofu! Hivi hamjui mlitoka katika kitu hicho miaka hamsini iliyopita, na

mkalirudisha kundi hili la watu moja kwa moja ndani yake? Hivi hamwezi kulisikia Neno la Bwana? Mifupa iliyokauka, mna shida gani? Hamtapokea kile mlichotumiwa. Wasingekipokea wakati huo, hawatakipokea sasa.

¹⁸⁸ Sasa, mnajua nini? Tena, kwa hiyo tena mipango yake na mipango ya ulimwengu wa dhehebu na kanuni za imani, zinaporomoka. Mipango ya mwanadamu inaporomoka. Mungu kamwe hakutupa kanuni za imani. Kamwe hakutupa dhehebu. Ninataka mtu fulani anionyeshe katika Biblia mahali alipofanya hivyo. Ninaweza kuwaonyesha mahali Yeye alipowaambia msifanye jambo hilo. Ninyi nionyeshe mahali aliposema mfanye hivyo. Mnasema, “Basi, Ndugu Branham, Yesu alimpa mwanadamu kitu gani?” Ufalme. Haleluya! Na Yeye ndiye Mfalme, Mfalme wa watakatifu, Bwana wa mabwana. Yeye alitupa Ufalme. Si mwanasiasa, mfumo wa kimadhehebu; bali Ufalme. Yeye alimwambia... Pilato, Pilato alisema, “Je! Wewe Ndiye Mfalme wa Wayahudi?”

¹⁸⁹ Akasema, “Ulisema hivyo.” Akasema, “Kama Ufalme Wangu ulikuwa ni wa ulimwengu huu, watu Wangu wangenipigania, bali Ufalme Wangu ni wa Juu.”

¹⁹⁰ Basi kwa nini sisi tuyashikilie mambo ya ulimwengu wakati sisi ni watoto wa Ufalme ambao ni wa Juu? Mnaona? Kuna kasoro mahali fulani. Lakini hatukupewa mfumo. Hatukupewa dhehebu, hatukupewa u—utawala wa kisiasa wa ulimwengu, bali tulipewa Ufalme wa unyenyekevu, kwa kuwa Uhai wa Mwana-Kondoo umo ndani yetu. Sio wa ulimwengu, ninyi si wa ulimwengu tena. “Watoto wadogo, ninyi si wa ulimwengu. Ninaomba, Baba, kwamba kama vile Mimi nisivyo wa ulimwengu, kwamba wao wasiwe wa ulimwengu.” Mnaona? Hilo ndilo Yesu alilotuomba. Hata hivyo tunageuka moja kwa moja na kujishikanisha wenyewe katika mifumo mle ndani ambamo watu wa kila aina wanaingizwa. Sasa, mnajua hakuna kanisa ulimwenguni ila lile lililojaa wanafiki. Na Yesu alisema, “Msijifungie nira miongoni mwa wasioamini.”

¹⁹¹ Kwa hiyo mbona kujifunga nira na dhehebu wakati umepewa Ufalme wa Mungu ambao unazaliwa ndani yake? Na hakuna mnafiki ndani yake! Wote ni safi, wana na binti za Mungu wasioghoishiwa, wanaoliamini Neno Lake kutoka Mwanzo hadi Ufunuo na wanadumu Nalo. Na maisha yako yanathibitisha jambo hilo, kisha Mungu anathibitisha Neno Lake kwake. Huyu Ndiye Masihi. Huyu ndiye Mke wa Masihi. Na Mungu anaweka kwenye mfumo huo waalimu, wachungaji, manabii, na kadhalika, apate kuweka Umasihi huo Wake moja kwa moja mle ndani, usiochanganywa na kanuni za imani za kimadhehebu, bali kinayang’oa mambo hayo na kuliweka Kanisa safi, lisiloghoshiwa kwa Kristo na Neno Lake.

¹⁹² Unafikiri kanisa litalipokea jambo hilo? Watalitupa nje. Hawataki uhusiano wowote na Hilo. Wana mfumo wao wenyewe

wa siasa. Na kama vile Marekani imepata mtu wao mwenye kipaji, vivyo hivyo kanisa litapata mtu wake mwenye kipaji. Litampata, ninyi angalieni tu. Yuko njiani sasa hivi. Tayari wamenjinyonganyonga wakaingia ndani yake.

¹⁹³ Lakini sisi tuna Ufalme, na katika Ufalme huu una Uzima wa Milele. Sio uanachama, bali Uzima wa Milele. Nao unatawaliwa na Mfalme wa Milele. Ufalme wa Milele uliojaa Uzima wa Milele, unaongozwa na Mfalme wa Milele, kwa watu wa Milele waliochaguliwa tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. “Kwa maana wale aliotangulia kuwajua, Yeye aliwaita; na hao aliowaita, aliwahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, Yeye amewatukuza,” Waebrania 11. Hiyo ni kweli.

¹⁹⁴ Sasa, inategemea unatarajia kitu gani. Kama wewe ni Ibrahimu, unautazamia Ufalme huo. Ninaweza kukuonyesha huo asubuhi ya leo. Naam, bwana. Sasa, Ufalme wa Milele uliojaa Uzima wa Milele, unaoongozwa na Mfalme wa Milele kwa Neno Lake la Milele, kwa watu wa Milele waliochaguliwa tangu zamani. Huo hapo. Mbona? Umekuwako daima, sikuzote utakuwako, kamwe haukuwa na mwanzo wala mwisho. Katika nia ya Mungu ulikuwa katika ninii hasa . . . wakati ulipokuwa na Mungu Milele. Na kusudi la Mungu litatekelezwa.

¹⁹⁵ Kwa hiyo, ulimwengu huu unaporomoka. Acha uporomoke, hilo ni sawa, utaporomoka hata hivyo. Mika alisema nini hapa, Mika alinena juu ya nini hapa? Milima itayeyuka, itatiririka kama nta na kumwagika kama m—mto wa barafu unaofoka, ama kitu kama chemchemi ya maji moto, hasa. Utayeyuka na kuanguka, bali Yehova atadumu milele. “Miili yote ni nyasi, pumzi ya Mungu inaipulizia kama ni ua, nyasi, ni zuri jinsi gani, inanyauka, bali Neno la Mungu litadumu milele,” Isaya 40 ilikuwa ikitabiri juu ya kuja kwa Masihi, ikasema hivyo. Kanuni zetu zote za imani, mifumo ya madhehebu, waalimu, wenye vipaji, na chochote kile, vitaangamia, bali Neno la Mungu litadumu milele. “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, milango ya kuzimu haiwezi kulishinda.”

¹⁹⁶ Tuko katika wakati wa Krismasi. Wala sikujua tulikuwa tukifikia wakati huu wa mchana. Ninapotea tu ninapowazia juu ya mahitaji ya wakati huu. Nitaharakisha. Naam. Nasi tumezaliwa katika Ufalme huu na tunaweza . . . sisi—sisi Wakristo tunaoamini na tulio katika Ufalme huu. Sasa, huku katika Kitabu cha—cha Waebrania, tulichosoma muda mfupi uliopita, “Kwa maana tunapokea Ufalme.” Sio kupokea kanuni ya imani, sio kupokea mfumo. “Tunapokea Ufalme usioweza kutikisika.” Ulimwengu unaporomoka. Hiyo ni kweli. Na kila mwanasiasa, kila dhehebu na kila kanisa vitaporomoka, bali tunapokea Ufalme usioweza kutikisika. “Kwa maana ikiwa wale waliomkataa Yeye aliyenena kutoka Mlima Sinai, na dunia ikatetemeka chini ya Sauti Yake, ni zaidi sana jinsi

gani mwone hamumkatai” (nani?) “Yeye, Neno Lake linalonena kutoka Mbinguni, kutoka kwenye Ufalme Wake, kwa kuwa tuko katika Ufalme usioweza kutikisika.” Amina. Kila kitu kilicho nje ya huo . . . Mungu alituma kila kitu, alikifanya dhaifu kipate kuvunjika. Katika hali yake ya udhaifu jinsi hiyo, hakina budi kuvunjika. Ni dhaifu. Lakini, kumbukeni ya kwamba sisi tuna Ufalme ulio imara sasa, wakati kila kitu kinapoanguka na kuachia. Si ajabu Eddie Perronet alisema, “Juu ya Kristo Mwamba wenye imara nasimama, ardhi zingine zote ni mchanga udidimiao.” Ufalme! Sio mfumo wa uanasisa, sio mfumo wa kisiasa, sio mfumo wa kanisa, sio mfumo wa kimadhehebu; yote yanakuwa ni Mafarisayo na madaktari wa ibilisi. Bali tunapokea Ufalme, Mfalme wa Milele ambaye ni Neno la Milele, ambaye yuna Uzima wa Milele; kwa Neno Lake la Milele kwa watu Wake wa Milele ambao wana Uzima wa Milele, nasi ni washirika wa huu. Loo, jamani! Jambo ndilo hilo.

¹⁹⁷ Sasa, chochote kinachokutoa kwenye Hilo ni kiovu, huyo ni masihi wa uongo, upako wa uongo. Loo, yeye alisema, “Huyo ndugu alikuwa na upako mwingi sana!” Ni upako wa aina gani? Jambo ndilo hilo. Hitler alikuwa na upako, pia. Khrushchev anao, pia. Papa Pius anao, pia. Una upako wa aina gani? Kama haujatiwa mafuta na Neno hili na unathibitisha kila Neno kwamba ni Kweli, achana nao. Uovu. Kama haujizai, basi haujarutubishwa. Utaonyesha rangi yake. Loo, mnasema, “Lakini huo ulikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine. Sisi . . .” Achana na kitu hicho. Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Naam, bwana.

¹⁹⁸ Kwa hiyo wakati ulimwengu huu unapoporomoka, tunazaliwa katika Ufalme usioweza kuporomoka. Je! mnaamini ulimwengu unaporomoka? Mifumo yake inaporomoka. Mnaamini hilo? Mnaamini m—mfumo wa uchumi unaporomoka? Mfumo wa kisiasa unaporomoka. Utaifa, mfumo wa U.M. unaporomoka. Kanisa linaporomoka. Madhehebu yanaporomoka. Kila kitu kinaporomoka. Lakini tuna Ufalme usioweza kutikisika, ni Ufalme wa Milele wa Mungu, hauwezi kutikisika.

¹⁹⁹ Tunaambiwa ya kwamba mfumo mpya wa dhehebu hili, wa kuleta hapa hili Baraza la Makanisa Ulimwenguni, utaleta amani duniani. Ni ku—kupuuzwa jinsi gani, ni ku—kukosoa kubaya namna gani usoni mwa Kristo! Ni ukosefu wa heshima ulioje, kukufuru kwa jinsi gani huko! Ni cha ibilisi. Ati mwanadamu anaweza kuratibu kitu vizuri kuliko Mungu anavyoweza kuwatumia? Mnara wa Babeli! Ni Babeli nyingine ambayo haina budi kuanguka. Ati amani duniani? Masihi wa uongo! Mpinga Kristo katika mafundisho yake. Utawezaje kuyaleta haya madhehebu pamoja wakati hata hayataninii . . . Hayawezi hata kukubaliana yenyewe kwa yenyewe sasa wakati yamevunjika katika mifumo midogo namna hiyo, vipi kuhusu

yote yakiungana pamoja na kwenda kule? Naam. Mnaona, ni njama ya uongo. Yote yamefanywa kuutupilia Uprotestanti katika Urumi. Ni fundisho la uongo la mpinga Kristo.

²⁰⁰ Ufalme wa Mungu si wa ulimwengu huu. Yesu alisema hivyo. “Ufalme wangu si wa ulimwengu huu.”

²⁰¹ Kwa hiyo kama ufalme huo umeundwa hapa ulimwenguni, ni masihi wa uongo, masihi huyu atakayetolewa kwa kanisa la Kiprotestanti hivi karibuni sana, ambaye watamchukua, kwa sababu wanamtazamia. Wanautafuta mfumo huu ambao unaweza kufanya, “Vema, sasa, sisi Wamethodisti na Wabaptisti, hakika, sisi—sisi kwa namna fulani tunakubaliana, unajua. Sisi—sisi Wapresbiteri, sisi Wapentekoste, loo, wana tofauti gani, ndugu?” Kuna tofauti! Mungu anawafanya tofauti. “Bali, vema, tunajitolea tu kwa jambo hili.” Na mafundisho yenu makuu ya kiinjilisti, mnayaachilia. Mtaingiaje mle pamoja na kundi la watu ambao hawaamini chochote, baadhi yao ni makafiri? Basi huyo ni masihi wa uongo. Hiyo ni kweli. Naam, bwana.

²⁰² Sasa, Ufalme wa Mungu si wa ulimwengu huu. Na wakati Kristo alipokuwa hapa, Yeye alitupa utaratibu wa Ufalme huu. Yeye alitupa utaratibu wa Ufalme wa Mungu, Ufalme wa Baba, ambao ni Neno Lake. Sasa, kama unataka kujua jinsi unavyoingia katika Ufalme huo, Neno hili lina hilo. Ukiingia kwa mlango mwingine wowote... Inakubidi kuingia katika mlango ule ule wengine walioingilia. Kama ukijaribu kufanya mlango mwingine, mbona, wewe ni kama mwizi na mnyang’anyi. Naye alisema, “Yeyote atakayeongeza neno moja kwa Hili, ama kuondoa Neno moja Kwake, huyo ataondolewa (sehemu yake) kutoka katika Kitabu cha Uzima.” Basi kama ukidai jina lako liko kwenye Kitabu cha Uzima, kama ulidai, usiache likatolewe.

²⁰³ Wakati, Petro kwenye Siku ya Pentekoste alipoufungua mlango wa kuingia katika Ufalme. Aliufungua. Ufalme ulikuwa ndio kwanza uanzishwe huko Yerusalemu. Ninataka mtu fulani aniambie ya kwamba Kanisa lilianzia huko Roma. Ninataka mtu fulani anithibitishie jambo hilo. Kanisa kamwe halikuanzia Roma, Kanisa lilianzia Yerusalemu. Ufalme ulianzishwa kwenye Siku ya Pentekoste. Na wakati wanadamu walipotaka kujua jinsi ya kuingia kwenye Ufalme huu, Petro alisema, “Tubuni, kila mmoja wenu, na mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Kwa kuwa huo ndio unaowaweka katika Ufalme huo. Sera nyingine yoyote, kupitia kwenye dhehebu ama kupeana mkono, ama chochote kile, ni masihi wa uongo. Hata iwe inapendwa na watu jinsi gani, na jinsi utakavyokuwa mtu mashuhuri, na huenda ukawa shemasi, hata mchungaji ama askofu, ama mzee wa kanisa ama mwangalizi wa jimbo, haidhuru wewe ni nani, ni ya uongo mpaka utakapomrudia Mwana-Kondoo mnyenyekevu wa Mungu na Ufalme Wake.

²⁰⁴ Sasa angalieni. Naye alitupa ratiba, Neno la Baba. Naye mwaminio wa kweli hulishikilia Hilo, maana hawezi kujisaidia, ni Ufalme wa Mungu ndani yake. Na kama vile Ibrahimu, yeye anaita chochote kinyume cha Neno la Mungu kana kwamba hakikuwepo. Na kama mtu yeyote akikwambia ya kwamba dhehebu ni la Mungu, wewe kaa kama vile Ibrahimu. Kama mtu yeyote akikwambia huna budi kunyunyiziwa, ama namna fulani ya kitu kidogo, mfumo ama kitu fulani kinyume cha Neno la Mungu, usikiamini. Kihasabu kana kwamba hakikuwapo. Kama wakisema, “Vema, sasa, mpenzi, haidhuru kwako kufanya *hivi*.” Usikiamini, wakati Mungu... Kasema, “Halidhuru kwa wanawake kukata nywele zao,” wakati Neno la Mungu linaposema ni chukizo Kwake, kufanya hivyo. Unaposema, “Mbona, ninavaa suruali za kike. Sivai kaptura.” Mungu alisema mwanamke atakayeava vazi limpasalo mwanamume, ni chukizo Kwake. Biblia ilisema ni makosa kwa mwanamke kukata nywele zake, hata si jambo la kawaida kwake kuomba na kadhalika namna hiyo. Hata huku kichwa chake hakijafunikwa, anakiaibisha kichwa chake mwenyewe. Mungu analikataza! Na mfumo huo unaokwambia ni sawa kufanya hivyo, usikiamini. Ni kutiwa mafuta kwa uongo. Ni kristo wa uongo. Ni kinyume na Neno la Mungu. Wenye haki wanalishikilia Neno la Mungu kwa sababu ndio mpango wa mfumo wa Mungu wa Milele.

²⁰⁵ Wakati Mungu alipomuumba mwanamume, Yeye alimuumba kwa njia moja. Alipomfanya mwanamke, alimfanya kwa njia nyingine... akamfanya kwa njia nyingine. Kuna maagano mawili mbalimbali, mipango miwili mbalimbali, tofauti mbili pamoja kati yao. Wala hawafanani. Hawafanani, hawapaswi kufanana kwa vitendo, wako tofauti kabisa. Nao wanawake wanajaribu kuwa kama mwanamume, na mwanamume amekuwa dondoadume sana amekuwa kama mwanamke. Nilimwona mvulana mmoja jana, huko Cincinnati, alionekana kama Bibi Kennedy, nywele hizo, jinsi zilivyokuwa namna hiyo. Mungu anamtaka mwanamume aonekane kama mwanamume! Anamtaka mwanamke aonekane kama mwanamke!

²⁰⁶ Nawaambia, mfumo huu wa Kiyezebeli wa ibilisi umeupotosha ulimwengu mzima, hakuna mahali pazuri ndani yake. Wote ni vidonda vinavyotoa usaha, vidonda vya kansa, donda ndugu la ibilisi ambalo linakula kiini chenyewe kutoka kwe—kwenye mifumo ambayo wameweka hapa. Shetani ni ndege mla mizoga anayeula ufalme wake mwenyewe. Yeye ni ibilisi, ni mchafu, yeye ni ba—baba wa uongo. Anakula miili ya watu wake mwenyewe. Ibilisi!

²⁰⁷ Kristo ndiye Mfalme wa mfalme na Bwana wa bwana, Masihi mtiwa mafuta. Mwaminio hulishikilia Neno hilo. Mungu na Neno Lake ni mmoja. Mimi na neno langu ni mmoja. Wewe na neno lako ni mmoja. Basi usiegeme, kutumia mawazo yako

mwenyewe; tumia wazo Lake, ndipo wewe ni sehemu ya Mungu kwa sababu wewe na Neno Lake mmekuwa mmoja. Unaona? Basi wewe umo ndani ya Ufalme huo.

208 Ibrahim aliita chochote kilichokuwa ni kinyume cha ahadi ya Mungu kana kwamba hakikuwako. Naam, yeye...kama vile mifumo ya kujibunia siku hizi, yeye angefanya jambo lilo hilo. Basi ukiwa katika ufalme wa namna hiyo...nitafunga, nitaacha baadhi ya mihtasari hii na kufunga. Angalieni, ni...Ukiwa katika Ufalme kama huo, inakuwaje? Sasa, huku kukemea kote, lakini kwa uchaji na heshima na uaminifu, kwa agizo nililopewa na Neno la Mungu, nililopewa na Roho Mtakatifu, kuliangalia kundi la kondoo ambalo Yeye ameniweka kulisimamia, nikiliheshimu, nikilishikilia haidhuru ni kitu gani kinakuja, kulitikisa tu kulia na kushoto na kukaa papa hapa na Neno hili. Hili limeagizwa. Basi kama tukiupokea Ufalme...

209 “Ndugu Branham, watu hawa wengine wote wanasema, ‘Wewe ni wa dhehebu gani?’”

Nasema, “Sina.”

“Wewe ni nani?”

“Kwa kuwa sisi tuko katika Ufalme.”

“Vema, mnakusanyika wapi katika huu? Mnaenda wapi?”

210 “Tunaketi katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu, tumeinuliwa katika Uwepo wa Mfalme wetu.” Ule Ufalme! Utukufu! Sasa ninaanza kujisikia kubarikiwa. Ufalme wa Mungu ambapo wanakutana pamoja, Roho Mtakatifu anawainua moja kwa moja katika Uwepo wa Mfalme, nasi tunaketi pamoja katika ulimwengu wa Roho tunapobatizwa katika Kristo Yesu. Huko ndiko kwetu.

211 Mke aliniambia tulipokuwa tukienda sokoni, niliwaambia, msimu uliopita wa kiangazi, tulimwona mama mmoja aliyekuwa amevaa rinda. Kilionekana kuwa ni kitu cha ajabu sana. Alionekana wa kigeni. Mnaona? Alisema, “Ni kwa nini? Tunawajua wanawake hawa. Baadhi yao wanaimba kwenye kwaya hapa.”

212 Loo, rafiki! Nitasema jambo hili, ingawa linarekodiwa, afadhali niliseme kwa vyovyote vile. Mwajua, nami ninasema hili kwa uchaji na heshima. Shikilieni tu hii. Mmewaona maelfu mara maelfu wakija jukwaani, na mmewaona kila mara wakija pale bila kukosea. Naye Ndugu Arganbright hapa anajua juu ya sehemu ya ulimwengu ambako tumekuwa, kwenye nchi za ng'ambo, hakuna hata wakati mmoja inashindwa ila ni kusema Kweli. Ninapoenda sehemu hizi na kuona hizi kwaya zenye majoho, hao wanawake na wanaume wamesimama pale wamevaa hayo majoho ya Golgotha, na kuwasikia wakiimba kama viumbe wa kimalaika; kwa Roho wa utambuzi nikiangalia huko chini, kama—kama ilinibidi asubuhi ya leo kwenda

kuwavuta watano wao kutoka kote ulimwenguni, ambao hawakuwa na hatia ya uchafu, sijui ningewapata wapi. Hilo ni tamshi kweli kweli, bali hiyo ni Kweli, Mungu anajua jambo hilo. Mkono wangu ukiwa hapa juu ya Biblia. Hiyo ni kweli, sijui ningewapata wapi. Mnaona, kama Mungu alisema, “Nenda ukawalete watano uwajuao.” Ningesema, “Sijui nitaenda wapi.” Loo, jamani! Mfumo wa jinsi hiyo! Uchafu wa jinsi hiyo!

²¹³ Hicho ndicho ulimwengu unachotaka. Hicho ndicho ulichotaka wakati huo, hicho ndicho unachotaka sasa. Hicho ndicho utakachopata sasa. Mtu akisimama pale, akiwa huko nje na mke wa mwanamume mwingine. Kunywa pombe, kuvuta sigara, huku amevaa joho, kufunika jambo hilo. Wazia, na Mungu anaona kupitia kwenye jani hilo la mtini. Huyu Hawa akisimama pale akiwa na hatia ya kutosha na uchafu moyoni mwake, pia, kama ungaligeuzwa kuwa maji, yangeuelesha mtumbwi. Na anasimama pale akiwa na kipaji alichokipata kimaumbile ya kawaida, kuimba, na kuishikilia sauti yake mpaka karibu, anakuwa mweusi usoni, akijaribu kuimba kama malaika ama kitu kama hicho, na chini ya hilo joho, kashifa, uchafu, kinyaa. Nawe unaweza kusimama mimbarani na kulisema, naye atainua midomo hiyo juu, iliyopakwa rangi, atoke humo jengoni, akisema, “Si lazima nisikilize upuuzi kama huo.” Lakini utapiga kiyowe kwa sauti kuu siku moja ukiomba huruma, katika kuzimu. Itakuwa umechelewa sana wakati huo. Wewe lipokee wakati ungali una nafasi ya kulipokea. Nawe! Loo, jamani!

²¹⁴ Lakini Kanisa linaupokea Ufalme ambao tunapoketi katika ulimwengu wa Roho na tumeinuliwa katika Uwepo wa Mungu, tukiketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, tukijua jambo hili, kwa uhakika wa imani, ya kwamba tuko katika Uwepo wa Mfalme aliyetiwa mafuta. Loo! Kuna Mbingu mpya zitakazokuja, na nchi mpya, na ambako hatutaachana tena mradi Umilele unadumu. Tunatazamia hizo Mbingu mpya na nchi mpya. Huu, unaweza kuuchukua wote unaotaka. Kwangu mimi, ninautaka Ule.

²¹⁵ Inategemea mawazo yako umeyaweka wapi. Inategemea umefungiwa kwenye nguzo gani. Ukijifungia kwenye nguzo yako ya kimadhehebu, utaporomoka moja kwa moja pamoja nayo. Kama ukijifungia kwenye kitu chochote cha ulimwengu huu, siasa zozote na kadhalika namna hiyo, na kuyatumaini hayo, utazama pamoja nayo.

²¹⁶ Lakini tumaini langu halijajengwa juu ya chochote ila Damu ya Yesu na haki Yake. Basi yote yanayoizunguka nafsi yangu yakitoweka, na kila mhudumu anikatae, na kila kanuni za imani zinifukuze, wala sina mahali hata pamoja pa kwenda, Yeye ndiye tumaini langu lote na ngome yangu. Juu ya Mwamba huo, juu ya Kristo ule Mwamba imara nasimama, ardhi zingine zozote ni mchanga udidimiao. Siku moja labda huenda nitazikwa

makaburini mahali fulani, huko ndani chini ya bahari, kwenye ajali ya ndege, niuawe katika ajali ya garimoshi ama motokaa, popote pale ambapo Mungu amenichagulia kwenda, ila jambo hili moja, ninajua jambo hili, ya kwamba nimetia nanga nafsi yangu katika Kimbilio la Raha huko ng'ambo, katika Neno Lake. Ninaamini hilo, kwamba hili hapana shaka ni Neno la Mungu.

²¹⁷ Mungu hana budi kuuhukumu ulimwengu kwa kitu fulani. Kama akiuhukumu kwa kanisa, atauhukumu kwa kanisa gani? Mbona, hakuna kitu cha kuuhukumia. Basi kuna Kitu kimoja tu kilichosalia, Neno Lake, Hilo ni la Milele, Hilo haliwezi kuongezewa wala kuondolewa.

²¹⁸ Nimetia nanga nafsi yangu mle, kwa urahisi wa kuweka mikono yangu juu ya Dhabihu yangu, nikikiri ya kwamba mimi si mwema hata kidogo. Hakuna kitu ndani yangu, Ee Bwana Mungu. Mtume huyo Masihi juu yangu na ubadilishe utu wangu uwe vile nilivyokuwa, na unifanye katika sura Yako Mwenyewe, jinsi ungependa niwe.

²¹⁹ Haijalishi ungaliuchoma mwili kiasi gani, jinsi gani ungalimwangamiza mtu, jinsi ungeongea dhidi yao, ama chochote anachosema, siku moja Yeye atatufufua tena. Na kuna Ufalme tunaupokea ambao hauwezi kutikiswa. Loo, jamani!

²²⁰ Pia, kumbukeni, katika mambo haya yote yenye utukufu tunayofurahia sasa, tukiketi katika ulimwengu wa Roho, ni utangulizi tu. Haleluya! Ni mwanzo wa yale yanayokuja. Huo ni utangulizi tu wa simfoni ijayo. Loo! Haleluya! Nena kuhusu huku kupaza sauti na kusifu, na kutukuza, na kumwinua Mwana-Kondoo! Siku moja wakati Malaika watakaposimama kuizunguka dunia, mpindiko wa dunia, wameinamisha vichwa, na kulisikia maskini kundi hilo dogo lililosafishwa kwa Damu likiimba hizo nyimbo za ukombozi wa Damu ya Yesu Kristo, Ee Mungu, ninataka kuunganishwa nao. Jalia nipachukue mahali pangu pamoja na Yeye sasa. Jalia nichukue dhamana yangu, Yesu ni wangu, nitamchukua Yeye na Neno Lake. Naam.

²²¹ Nikifunga, nataka kusimulia hadithi hii fupi kwa ajili ya Krismasi, kusudi watoto waweze kuishika. Na kama nimewauzidi kwa kukaa kwa muda mrefu zaidi. . .Maskini msichana mmoja jana. . .Ndugu Brown alihubiri karibu saa moja, somo zuri sana, yule mtu aliyetiwa mafuta. Msichana akasema, "Ni kwamba tu aliwashikilia muda mrefu sana." Paulo alihubiri usiku kucha. Waliketi pale mpaka wakaingiwa na usingizi mzito, na labda wakiketi saa baada ya saa, ndipo jamaa mmoja akaanguka na kujiua. Naye Paulo akajinyosha tu juu yake, akasema, "Msihofu." Sikilizeni tu jambo lifaalo.

²²² Kulikuwako na mzee fundi viatu, nami naamini ilikuwa ni Ujerumani ambako a—angetengeneza viatu vyao. Basi siku moja wakati. . .Katika wakati wake usio wa kazi alikuwa akiichukua Biblia, naye angeisoma. Angesoma fungu na somo

la Maandiko, naye akawa mnyofu sana. Akasema, “Unajua,” akasema, “Mimi—mimi...wakati Krismasi hii itakapokuja, sitauwasha mti wowote wa Krismasi.” Lakini akasema, “Mnajua nini?” Akasema, “Nitaandaa chakula ki—kingi cha jioni, nami nitapika ninii yangu...nitambanika mwana-kondoo wangu na nitachuma forsadi zangu, na supu yangu yote na kadhalika.” Naye alikuwa tu amezama kwenye mawazo. Kisha akasema, “Nitakiandaa mezani nami nitamwalika Yesu aje aketi upande wa pili pamoja nami mezani. Ninataka kumjua Masihi wa Mungu na kile ninachoweza kufanya kwa heshima.” Akasema, “Ni—nitafanya haya yote. Na kisha nitakaa mezani na nitakiombea chakula, nami nitamshukuru Mungu kwa yale amenipa. Na halafu nitasema, ‘Bwana Yesu, waweza kuja na kuketi upande wa pili hapa, kwa ajili tu ya chakula cha jioni cha Krismasi pamoja nami?’”

²²³ Urahisi, Mungu daima huusikia huo, unyofu. Basi mzee huyo mshona viatu akaweka akiba fedha zake kuandaa chakula kama hicho, mwajua, naye angemwalika Mfalme wa wafalme. Ndipo akakiandaa, naye akakipika, kisha akakiweka mezani. Naye akajiosha vizuri sana, na—na kuvalia nadhifu, na akachana nywele zake. Na akaketi mezani, kisha akaweka kiti cha Yesu, na akaweka viti vingine pale. “Huenda vikawa ni kwa ajili ya mitume,” akasema, “ikiwa labda watakuja.”

²²⁴ Kwa hiyo mzee huyo akainamisha kichwa chake akaomba baraka, na—na kumshukuru Mungu kwa chakula hicho. Ndipo akasema, “Sasa, Yesu, waweza kuja na kula pamoja nami chakula cha jioni cha Krismasi hii?” Ndipo akaanza kula huku akikiangalia kile kiti. Hakuna mtu aliyekuja. Akala kidogo zaidi, kisha akasema, “Bwana Mungu, nimekualika nyumbani mwangu. Waweza kuja na kuwa pamoja nami?” Basi akaanza kunyosha mkono apate kumega chakula, ndipo mtu fulani akabisha mlangoni.

²²⁵ Basi akaenda mlangoni. Alikuwa ni mzee, mabega yameinama, amevaa nguo zilizoraruka. Akasema, “Samahani bwana, ninasikia baridi, je! waweza kuniruhusu nipate joto?”

²²⁶ Naye akasema, “Ingia ndani.” Basi akaingia na kusikia harufu hiyo nzuri ya chakula, kwa namna fulani mate yakajaa kinywani, akageuka. Kasema, “Waweza kuketi?” Kasema, “Ninatarajia wageni, lakini waweza kuketi na ule tu pamoja nami mpaka wageni watakapokuja?”

²²⁷ Akasema, “Asante. Ningefurahi kufanya hivyo.” Ndipo akaketi, nao wakala chakula cha jioni. Mzee huyo akamshukuru, akaamka na kwenda.

²²⁸ Fu—fundi viatu huyo akageuka, akasema, “Bwana Mungu, kwa nini ukanivunja moyo?” Kasema, “Niliandaa kila kitu. Nilifanya yote niliyojua kufanya.” Laiti ungalifanya hivyo! “Nilifanya yote nijuaayo jinsi ya kufanya, na nikawazia ungeingia

na kula pamoja nami.” Ndipo akaanza kulia, na akakimbia akaanguka kitandani. Naye alikuwa amelala pale kitandani, akilia. “Ni—ni—nilifanya yote niliyodhani yalikuwa ni sawa, Bwana, basi kwa nini Wewe hukuja kula pamoja nami?”

²²⁹ Ndipo sauti ikamjia, naye akayakumbuka Maandiko, “Kadiri mlivyowafanyia walio wadogo wa hawa watoto Wangu, mmenitendea Mimi.”

²³⁰ Naam, Irene. . . Samahani, ilikuwa ni Mtakatifu Martin. Siku moja yenye baridi kabla ya Krismasi, maskini ombaomba mmoja alikuwa amelala mtaani, akiganda kwa baridi. Watu waliokuwa na uwezo wangepitia pale, nao wakamwanguka tu maskini ombaomba huyo. “Vema, hana faida yoyote, yeye ni ombaomba tu. Mwache alale hapo.” Basi Martin akasimama na kuangalia aone kama baadhi ya watu ambao wangukiweza wangemsaidia, bali hakuona.

²³¹ Hatimaye, Martin mwenyewe hakuwa. . . ye—yeye alimwamini Mungu, bali alikuwa ni mwanajeshi. Alikuwa tu na koti moja. Akasema, “Kama mzee huyu akilala hivyo, ataganda hata afe.” Kwa hiyo akauchukua upanga wake na kulipasua koti lake nusu vipande viwili, akaenda akamfunika huyo mzee ombaomba nalo, na kusema, “Lala kwa amani, ndugu yangu.” Akaenda zake.

²³² Basi usiku huo kwenye kambi ya jeshi, akiisha kupiga rangi buti zake na kujilaza chini, alishikwa na usingizi. Ndipo sauti ikamwamsha. Akaangalia, akisimama mbele yake, na hapo alisimama Yesu amefunika kwenye maskini kile kipande cha koti ambacho alikuwa amemfunika nacho yule ombaomba.

²³³ Ninaweza kufanya nini basi katika mambo haya? Ninapaswa kufanya nini na mambo haya ninayojua ni ya kweli, mambo haya ambayo yamethibitishwa na kuhakikishwa ni ya kweli? Ninaweza kufanya kitu gani? Kulifunika Kanisa, si katika kanuni za imani wala dhehebu, bali katika Damu ya Bwana Yesu Kristo kwa Neno Lake. Kwa hiyo Yesu alisema, “Mliyowatendea hawa, mmenitendea Mimi.”

Na tuombe.

²³⁴ Bwana Yesu, kama ungalikuwa umesimama hapa asubuhi ya leo, Bwana. . . Ninajua unasimama, katika umbo la roho. Lakini kama ulikuwa umesimama hapa, kimwili, sidhani ningebadilisha somo langu hata kidogo. Ninaamini ningalisema mambo yayo hayo tu. Pia naamini, Baba wa Mbinguni, ya kwamba watu hawa ambao wamekaa bila chakula chao cha kawaida, kwamba wameketi hapa na kuisikiliza sauti ya mkwaruzo iliyochooka, bali kama ungalikuwa umesimama hapa, wasingekaa tena, kwa kuwa wanaamini ya kwamba Wewe upo hapa, kwa kuwa ni Neno Lako. Inaonyesha ya kwamba wanakupenda.

²³⁵ Tunashukuru sana kwa ajili ya kuzuriwa huku kwa Krismasi hii na Roho Mtakatifu ambaye hutuongoza na kutuonyesha kwamba Krismasi ni nini. Tunapooona ya kwamba ulimwengu unaporomoka, mifumo yake inavunjika. Lakini tuna furaha sana, tunashukuru sana kwamba tuna Ufalme na tunaye Mfalme, wala hauwezi kutikiswa. Na wakati hakutakuwako na ulimwengu tena, wakati hakuna siasa tena, wakati hakuna mataifa tena, Mungu ataanzisha Ufalme Wake nao wenye haki watatawala pamoja Naye. Wale ambao wameteseka hawatateseka tena.

²³⁶ Tusaidie, Bwana, kwenye msimu huu wa Krismasi, kukumbuka kile Masihi aliyetiwa mafuta kinamaanisha. Tusaidie kuelewa.

²³⁷ Bariiki hili, kusanyiko letu. Uwe pamoja nao, Baba yetu, na uwape haki na amani katika Roho Mtakatifu. Mbariki mchungaji wetu. Bwana, tunampenda. Mtumishi huyu shujaa anasimama tu akiwa ni mwaminifu. Na, akizungumza hivi majuzi usiku, alisema, “Mimi hapa, karibu na umri wa miaka sitini.” Wana watoto wadogo sana. Lakini kumbuka, jalia akumbuke jambo hili, Bwana, ya kwamba hakuna kitu kinachoweza kumwondoa kutoka hapa mpaka utakapokuwa tayari. Kama ukikawia, ninaomba ya kwamba ataishi kuwaona watoto wake wote wamefunga ndoa na kuwa na makazi yao wenyewe. Mbariki maskini mke wake wa thamani, maskini mjakazi Wako. Wabariki mashemasi wetu na wadhamini wetu.

²³⁸ Na, Mungu, ninashukuru Krismasi hii kwa ajili ya hawa wote, marafiki wangu wanaosafiri kupitia kwenye theluji, na kupitia kwenye barabara zinazoteleza na katika mvua, na kuchukua riziki zao na kuja mamia na mamia ya maili. Mungu, sijui niseme nini zaidi. Ninatumaini ya kwamba utafunua hayo mengine, yaliyo moyoni mwangu. Na jalia sikuzote niwe mwaminifu, Mungu, kwa Ufalme huu ambao umetuweka ndani. Jalia kamwe nisipatane, la, kulia wala kushoto. Ninakumbuka vema wakati uliponiambia wakati huo, “Usiende mkono wa kulia wala wa kushoto, ndipo njia zako zitafanikiwa. Ndipo utakapostawi vizuri.” Labda si katika mtazamo wa ulimwengu. Na sijali vile ulimwengu unavyowazia, ninataka kujua kile unachotaka, Bwana. Shauku Yako ndiyo ninii yetu... Mapenzi Yako ndiyo shauku yetu. Loo, shauku Yako iliyo ndogo sana ni—ni amri ya maisha kwetu, Bwana. Tunasimama kama Kanisa Lako.

²³⁹ Tusamehe sasa kwa yale yaliyotukia kote katika mwaka huu, mambo mabaya ambayo tumefanya na mahali tuliposhindwa katika sehemu nyingi sana, na ututie nguvu, Bwana. Na jalia sisi, kwenye wakati huu wa kusherehekea Krismasi, jalia tumfungulie Masihi mioyo yetu, mtiwa mafuta wa Mungu. Jalia aingie maishani mwetu na kututia mafuta, na kuishi mapenzi

Yake na kuuleta Ufalme Wake kutimia kupitia maisha yetu. Tudumishe vyema, wenye afya.

²⁴⁰ Mbariki maskini rafiki huyu wangu shujaa anayeketi karibu nami, Ndugu Arganbright. Ee Mungu, jinsi ambavyo umekuwa pamoja naye, na jinsi moyo wake umedhalilishwa na kupondwapondwa mara nyingi sana, bali tungali tunaamini amerutubishwa na Uzima wa Milele. Mbariki maskini mke wake. Ninawazia juu ya Bud, na Fred, mimi mwenyewe, Ee Mungu, jinsi ambavyo tumekuwa na ushirika huu mzuri sana.

²⁴¹ Tunaomba ya kwamba utatubariki pamoja sasa. Libariki kanisa letu dogo, watu hawa wote wa thamani. Na siku moja, Bwana, tunapokuwa ninii sana... tunataka macho yetu yawe safi sana kutokana na mambo ya ulimwengu hata tunaweza tu kumwona Mungu na Ufalme Wake, kusudi siku moja tuwasilishwe mbele ya Kristo, bila lawama, bikira safi, sehemu ya lile Kanisa kuu litakalokuja mbele Zake.

²⁴² Na halafu tutaungojea wakati ambapo utauanzisha Ufalme Wako hapa duniani, watu wanaoonekana kwa macho wakiwa na nyumba zinazoonekana, nao hawatapanda mwingine akala, bali wataishi Milele. Mpaka wakati huo, jalia tuwe nuru iliyowekwa juu ya kilima, mshumaa unaotoa mwanga kwa kila kitu kinachotuzunguka, kwa maisha yenye haki, yaliyotakaswa kwa Damu ya Kristo. Tujalie, Baba. Katika Jina la Yesu tunaomba.

²⁴³ Na, Bwana, juu ya lesa hizi, baada ya kuwaombea wagonjwa na kuwawekea mikono yetu, tukijiunganisha pamoja nao, ninaweka mikono yangu juu ya lesa hizi, nikiunganisha maombi yangu kwa Mungu. Na pamoja na lesa hizi na pamoja na watu hawa, Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe utaponya kila mmoja wa watu hawa ambao lesa hizi zinawawakilisha. Jalia wawe na afya na nguvu katika mwaka wote ujao, Baba. Kwa heshima na utukufu wa Mungu, tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²⁴⁴ Sasa wakati tukiuibimba tena, hebu na tupeane mikono na mtu fulani karibu nasi. Bakini tu, mkisema:

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza...

Ndugu Arganbright, hii ni...?...[Ndugu Branham anaendelea kupeana mikono—Mh.]

Sasa huku tukimwinulia mikono Yetu.

Nampenda, (kwa sauti kubwa sana sasa)
nampenda (namna hiyo)
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²⁴⁵ Na sasa pamoja na neno hili, pamoja, sisi sote tuseme hivyo. Tunapokea Ufalme [Kusanyiko linarudia, “Tunapokea Ufalme”—Mh.] usioweza kutikiswa [“usioweza kutikiswa!”]. Amina!

²⁴⁶ Sasa hebu na tusimame. Sasa, tuinue mikono yetu na mioyo yetu kwa Mungu, na shukrani sasa, halisi, mioyo yetu yote, “Nampenda!” Na tumwonyeshe Yeye wakati huu wa Krismasi.

Nampenda, nampenda
Kwani . . .
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²⁴⁷ Ibada ya ubatizo mara moja itaufuata huu. Nanyi ambao hamna budi kuondoka, tunashukuru ya kwamba mlikuwa hapa, na naomba daima mbaki katika Ufalme huo usioweza kutikiswa. Wakati tukiinamisha vichwa vyetu kwa dakika moja kwa maombi, nitamwomba Ndugu yetu wa thamani Arganbright kama atakuja hapa na kuruhusu wasikilizaji hawa wafumukane kwa maombi.



KUPOROMOKA KWA ULIMWENGU SWA62-1216

(The Falling Apart Of The World)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 16 Desemba, 1962, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org